# Nipashe

Jumamosi Novemba 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580413

www.ippmedia.com

MWANGA WA J...

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.inst...m.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**Walimu** watano kortini tuhuma kuvujisha mitihani

UKURASA 3



**Polisi** waliofukuzwa kazi wadaiwa kuuawa tukio la ujambazi

UKURASA 4

**Arteta: Pepe amemaliza hasira zangu**

UKURASA 20

# Kizungumkuti Viti Maalum CHADEMA

• **NEC** yasema ilipokea majina toka kwa Katibu Mkuu, Kamati Kuu yajichimbia kuwajadili kina Mdee, wenyewe wakacha kuhojiwa... *Endelea ukurasa 2*




Wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiwa wamekusanyika na mabango, nje ya ofisi za makao makuu ya chama hicho, Mtaa wa Ufipa, Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, wakiishinikiza Kamati Kuu ya chama hicho, kuwafukuza wabunge wa viti maalum 19 walioapishwa bungeni hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**BILIONEA MADINI AMTAJA MAGUFULI**

MCHIMBAJI mdogo wa madini kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai, Gabriel Laiser...

UKURASA WA 7

**NDUGAI ATAJA MWAROBAINI TATIZO LA AJIRA KWA VIJANA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema njia kubwa ya kumaliza tatizo la ajira miongoni...

## Serikali yaajiri walimu 13,000

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# TAKUKURU yazitaja UDSM, UDOM vinara rushwa ngono

UK. 2


**MICHEZO** **YANGA YATAMBA KUENDELEZA DOZI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Kizungumkuti Viti Maalum CHADEMA

**Na Romana Mallya**

SUALA la ubunge wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni kizungumkuti baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutoa ushahidi wa barua ya orodha ya wanachama waliopendekezwa na chama hicho kwenye nafasi hizo.

Wakati hayo yakijiri kamati Kuu ya CHADEMA jana ilikutana na kujifungia jijini Dar es Salaam kuwajadili wabunge hao 19, huku wao wakikacha kutokea kwa ajili ya kuhojiwa kama walivyokuwa wametakiwa kufanya hivyo.

Wabunge hao ni Halima Mdee, Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Peresso, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

Wengine ambao ni wabunge wapya ni Angesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau na Stela Fiyao ambao kwa pamoja hakuna aliyejitokeza mbele ya kamati hiyo ili kuhojiwa.

NEC kupitia taarifa yake jana iliyotiwa saini na Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Charles, ilibainisha kupokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, ikiwa na orodha ya majina ya wanachama wa chama hicho waliopendekezwa kuwa wabunge wa viti maalum.

Hivi karibuni, baada ya Mdee na wenzake kula kiapo mbele ya Spika mapema wiki hii jijini Dodoma, Mnyika aliibuka na kusema hawatambui wabunge hao kwa kuwa hawana baraka za chama na kwamba huo ni usaliti.

Taarifa hiyo ya tume ilikiri kupokea barua ya Katibu Mkuu wa CHADEMA yenye kumbukumbu namna C/HQ/ADM/20/Tu/05//141 ya Novemba 19, ambayo iliwasilisha majina ya wanachama waliopendekezwa kuteuliwa kuwa wabunge wa Viti Maalum. "Tume ilitumia orodha iliyowasilishwa na CHADEMA kuteua wabunge wa viti maalum hivyo. Wabunge wa Viti Maalum wa CHADEMA waliteuliwa kwa kuzingatia taratibu zote za kikatiba na kisheria," ilisema taarifa hiyo.

Dk. Charles alisema kuna taarifa zinasambaa kwenye mitandao kuwa tume imeteua wabunge wa CHADEMA ambao majina yao hayakuwasilishwa kwa kuzingatia taratibu.

"Mapendekezo ya wabunge wa Viti Maalum kwa CHADEMA yaliwasilishwa tume kwa barua, Novemba 20 tume katika kikao chake iliteua wabunge na madiwani wanawake wa viti maalum kwa kuzingatia matakwa ya katiba na sheria," alisema. Dk. Charles alisema kuanzia Septemba 26, tume ilikuwa ikipokea barua kwa vyama mbalimbali, barua zenye mapendekezo ya wabunge hao na Septemba 26, ilipokea barua ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ya CHADEMA ilipokewa Novemba 19.

KUHOJIWA KAMATI KUU

Jana, CHADEMA iliitisha kikao cha Kamati Kuu kwa ajili ya kuwahoji wabunge hao lakini katika hali isiyotarajiwa hakuna hata mmoja aliyejitokeza.

Kikao hicho cha Kamati Kuu ambacho kiliongozwa na Mwenyekiti wa Taifa CHADEMA, Freeman Mbowe, kilianza asubuhi huku Mdee na wenzake 18 wakigoma kwenda kama walivyotakiwa kupitia barua za wito ambazo chama kilidai iliwapelekea.

Katika kikao hicho wajumbe wawili ambao ni Tundu Lissu na Ezekiel Wenje wakishiriki kwa njia ya mtandao. Awali, kikao hicho kilipangwa kufanyika Makao Makuu ya chama hicho na wabunge hao walitakiwa kufika asubuhi lakini hadi uamuzi wa kubadili eneo kwenda hotelini kufanyika hakuna mbunge wa Viti Maalum aliyejitokeza.

Katika ofisi za chama mmoja wa wanachama alionekana akiwa amebeba bango linalosomeka, 'Kamati Kuu Fukuzeni Hao Covid 19'.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Brigedia Jenerali John Mbungo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha jana, baada ya kuokoa zaidi ya Sh. milioni 294 marejesho ya madeni ya vyama vya ushirika na madai binafsi yaliyotokana na dhuluma na utapeli. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# UDSM na UDOM zatajwa vinara rushwa ya ngono

**Na Beatrice Shayo**

UTAFITI uliofanywa kwenye baadhi ya vyuo vikuu nchini, umebaini kushamiri kwa rushwa ya ngoni huku Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho ni kikongwe nchini kuliko vyote na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) vikitajwa kuwa vinara wa vitendo

Aidha, utafiti huo umeanika shuhuda za waathiriwa wa vitendo hivyo huku ikibainika kuwa baadhi ya watuhumiwa hawajachukuliwa hatua zilizoshauriwa kuchukuliwa utafiti huo ulifanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Akisoma ripoti hiyo jana jijini Dar es Salaam, Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Denis Lekayo, alisema utafiti huo uliofanywa kwa kipindi cha Januari na Februari, mwaka huu.

"Vyuo hivi vilihusishwa katika utafiti huu kutokana na historia ya vyuo hivi, umiliki wake (vyuo vya umma) na wingi wa udahili wa wanafunzi. Hivi ndivyo vyuo vikuu vikubwa viwili vinavyomilikiwa na serikali na vinavyoongoza kwa kudahili wanafunzi wengi zaidi nchini," alisema Lekayo.

Alisema kutokana na ukubwa wake na idadi kubwa ya wanafunzi nchini, utafiti uliona kuwa ni sehemu sahihi ya kuweza kuchunguza na kujenga msingi wa kisayansi kuhusu rushwa ya ngono nchini.

Lekayo alisema walihojiwa watu 589 Kati ya hao UDSM 352 na UDOM 237. Utafiti huu umetumia mbinu ya uchunguzi lifani (case study) kwa lengo la kupata taarifa za kina rushwa ya ngono inavyotendeka katika taasisi za elimu ya juu.

Alisema matokeo ya utafiti yanaonyesha wanafunzi waliohojiwa asilimia 81.6 na Watumishi 91.4 walikuwa na uelewa wa dhana ya rushwa ya ngono.

Kwa mujibu wa Llekayo, matokeo yanaonyesha zaidi ya asilimia 50 ya waliohojiwa walieleza uwapo wa rushwa ya ngono katika vyuo vikuu vilivyofanyiwa utafiti. Matokeo hayo yanamaanisha kwamba rushwa ya ngono ni tatizo katika vyuo vikuu hivyo.

Aidha, alisema utafiti huo ulitaka kujua sababu zinazochochea rushwa ya ngono katika vyuo vikuu kwa kuwataja wahojiwa kueleza chanzo cha kuwapo vitendo vya rushwa ya ngono.

" Matokeo katika vyuo vyote viwili vilivyotafitiwa yanaonyesha kuwapo kwa sababu tano ambazo ni ukosefu wa maadili, ushawishi wa mtu mwenye mamlaka, mfumo wa utoaji taarifa kutokuwa rafiki, mifumo dhaifu ya kushughulisha rushwa ya ngono na mamlaka ya kutoa alama za mitihani kuachwa chini ya waliku pekee," alisema

Alisema katika utafiti huo wamebaini matumizi mabaya ya madaraka ili kujinufaisha kingono isivyo halali, uadilifu mdogo katika uongozi na kamati za maadili.

"Watu wa kamati ya maadili wao wenyewe wanafanya vitu ambavyo vinawafanya watu wasiwaamini na kuna mhadhiri ana ushawishi mkubwa katika kutenda vitendo vya rushwa ya ngono. Mara nyingi malalamiko yanayopelekwa hayashughulikiwi," alieleza aliyehojiwa.

Alisema ukosefu wa maadili kwa baadhi ya viongozi na wajumbe wa kamati za maadili kunatajwa kusababisha kukosekana kwa uwajibikaji jambo linalosababisha watumishi na wanafunzi kupoteza imani kwa uongozi wa kamati hizo.

Pia alisema wanataaluma wahadhiri wapya wanatambua kuwapo kwa mwongozo na kanuni za maadili licha ya kudai kutoziona kutokana na upatikanaji wake kutokuwa rahisi.

"Hali hii ilidhihirika wakati wa utafiti ambao ulikuwa vigumu kupata nyaraka hizi zinazosimamia sera, mifumo na muongozo. Wakati wa utafiti ilibainika nyaraka hizi hupatikana wakati mtumishi au mhadhiri anapopata matatizo ya kimaadili," alisema Lekayo.

Lekayo alisema kitendo cha kuvuja kwa taarifa, kumesababisha waathirika wengi kuwa waoga kutoa taarifa pale wanapobainika au wanapoombwa rushwa ya ngono.

Alisema vitendo vya rushwa ya ngono vinakiuka kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 kinachokataza rushwa ya ngono.

Alisema mtumishi yeyote wa chuo kikuu mwenye mamlaka au madaraka anayetumia nafasi yake kumwekea kigezo cha kupewa ngono na mwanafunzi au mtumishi mwenzake anayetaka huduma anakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Lekayo alisema alisema utafiti ulilenga kubaini njia na mbinu zilizotumiwa kufanya ushawishi wa rushwa ya ngono katika tasisi za elimu ya juu.

Alisema matokeo yanaonyesha kuwa mbinu ya utoaji wa alama za chini kwenye mitihani iliongoza kwa kutajwa na wahojiwa ikifuatiwa na vitisho vya kutofaulu kwa wanafunzi.

"Taarifa za kitaaluma zinaonyesha kuwapo kwa vitisho vya baadhi ya wahadhiri vya kutoa alama za chini kwa wanafunzi kama mbinu ya kuomba rushwa ya ngono. Wahadhiri wanajua kwamba mwanafunzi anakuja chuoni na lengo kuu kupata tuzo za kitaalamu," alisema

Lekayo alisema wahadhiri hutumia mwanya huo kwa kuwapa alama ndogo za masomo, kubadilisha alama za ufaulu, kuwafelisha au kuzuia matokeo yao ili kuandaa mazingira ya kuwashawishi kingono.

"Kwa ujumla utafiti umebaini tatizo la rushwa ya ngono kwenye vyuo viliyoshiriki lipo na kwamba tatizo hilo ni kubwa na si la kupuuzwa. Shuhuda za waathiriwa wa rushwa ya ngono pamoja na shuhuda za uwepo wa watuhumiwa ambao hawajachukuliwa hatua zilizotolewa," alisema.

Alisema utafiti umebaini kuwepo kwa sera, miongozo na sheria ndogondogo zinazoharamisha rushwa ya ngono kwenye taasisi zote za umma ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu mfano kumtaka mwajiriwa kufanya naye ngono kama kigezo cha kupendelewa kazini.

Lekayo alisema vyuo vyote viwili vina kanuni za maadili za watumishi ambazo zinabatilisha na kutoa katazo la kutumia rushwa ya ngono kutoa ufaulu, kufanya vitendo vinavyoashiria ngono au kufanya mawasiliano yanayoashiria uhitaji wa rushwa ya ngono.

Aidha, alisema utafiti umebaini mianya mingine inayosababisha kuendelezwa rushwa ya ngono ikiwa ni pamoja na ukosefu wa huduma za msingi kwa wanafunzi kama vile nyumba za kulala, mikopo pamoja na mifumo ya ajira za wakufunzi isiyozingatia weledi na maadili ya kazi kwenye taasisi za elimu.

**HABARI KITAIFA**

# Walimu kortini tuhuma kuvujisha mitihani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WALIMU watano wa shule za msingi mkoani Kilimanjaro, wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuvujisha mtihani wa darasa la saba na kusababisha matokeo ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Siashimbwe kufutwa.

Walimu hao waliofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi ni Philip Karenga, Fredrick Lyaruu, Florah Maambo, Elionora Shirima na Eutika Tesha.

Kesi hiyo ya jinai namba 473 ilifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Naomi Mwerinde, huku Jamhuri ikiwakilishwa na mwanasheria wake, Nitike Emmanuel. Emmanuel alidai mbele ya Hakimu Mwerinde kuwa walimu hao wanashtakiwa kwa mambo manne, la kwanza likiwa kushindwa kutunza karatasi za mtihani wa darasa la saba.

Alidai kuwa shtaka hilo linawahusu watuhumiwa wote watano ambalo ni kinyume cha kifungu cha sheria namba 20 kifungu kidogo cha kwanza na sheria namba 24 kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Baraza la Mitihani Sura namba 107 marejeo ya mwaka 2009.

Alidai kuwa Oktoba 7, mwaka huu, katika Shule ya Msingi Siashimbwe wilayani Moshi, kwa pamoja walitoa mtihani wa darasa la saba wa somo la Hisabati katika chumba cha mtihani wakijua kabisa kufanya hivyo ni kosa.

Shtaka la pili, kwa mujibu wa Emmanuel, pia linawahusu watuhumiwa wote la kushindwa kutunza nyaraka za mtihani wa darasa la saba kinyume na kifungu cha sheria namba 20 kifungu kidogo cha kwanza na sheria namba 24 kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Baraza la Mitihani sura namba 107 marejeo ya mwaka 2009.

Katika shtaka hilo, alidai kwamba Oktoba 7, mwaka huu, katika maeneo ya Shule ya Msingi Siashimbwe iliyoko Uru Shimbwe wilayani Moshi, washtakiwa walitoa mtihani wa darasa la saba wa somo la Kiswahili katika chumba cha mtihani, kitendo ambacho ni kinyume na sheria.

Shtaka la tatu, alidai kuwa linamhusu mshtakiwa wa kwanza, Philip Karengi, la kumiliki nyaraka ambayo ilikuwa imezuiliwa kisheria kinyume cha Sheria ya Baraza la Taifa la Mitihani.

Mshtakiwa huyo alidaiwa kuwa Oktoba 7, katika maeneo ya Shule ya Msingi Siashimbwe, alikutwa akimiliki karatasi ya majibu ya mtihani wa darasa la saba somo la Kiswahili, huku akitambua kuwa ni kosa kisheria.

# Serikali yamwaga ajira 13,000 za walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeajiri walimu wapya 13,000 wa shule za msingi na sekondari, wakiwamo walimu wa Sanaa, sayansi, mafundi sanifu wa maabara za shule.

Walimu hao wametakiwa kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi ndani ya siku 14, huku wakitakiwa kujaza mikataba ya kutohama kwenye halmashauri walizopangwa hadi watakapotimiza miaka mitatu ya utumishi.

Hatua ya kuajiri walimu hao, imetokana na kibali alichokitoa Rais John Magufuli Septemba 7, mwaka huu.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Joseph Nyamhanga (pichani), alisema jana kuwa walimu hao waliokidhi vigezo wamepangiwa kwenye vituo vyao vya kazi. Alisema walimu hao, wa shule za msingi ni asilimia 60 ya idadi hiyo huku wa sekondari wakiwa asilimia 40.

Mhandisi Nyamhanga aliwataka waliopata walimu hao kuripoti na kufanya kazi kwenye vituo walivyopangiwa na siyo kukaa katika makao makuu ya halmashauri.



"Mwalimu au Fundi Sanifu wa Maabara atakayechukua posho ya kujikimu na baadaye asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, atashitakiwa kwa kosa la kujipatia fedha au mali kwa njia ya udanganyifu," alisema.

Nyamhanga alisisitiza kuwa waajiriwa hao wapya hawatabadilishiwa vituo vya kazi walivyopangiwa kwa kipindi cha miaka mitatu na wanatakiwa kujaza mikataba ya kutohama halmashauri.

Aidha, aliwataka walimu hao kuripoti kwenye ofisi za wakurugenzi wa halmshauri, zinazosimamia shule walizopangiwa na kwenye shule husika kuanzia Desemba Mosi hadi 14, wakiwa na vyeti halisi vinavyotakiwa.

Vilevile, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zilizopangiwa walimu hao kuwapokea na kuwawezesha kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma.

"Wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa wakamilishe taratibu za ajira haraka ili walimu wapya waingizwe kwenye mfumo wa malipo. Wale ambao hawataripoti kwa muda uliopangwa nafasi zao zitajazwa na wengine ambao wapo kwenye kanzi data wanasubiri,"alisema Mhandisi Nyamhanga.

Aidha, alisema walimu 1,100 wenye shahada ya masomo ya sanaa walioajiriwa kwenye shule za msingi mishahara yao watalipwa kama walimu wa sekondari.

Alibainisha katika ajira hizo, walimu kwa ajili ya shule zenye mahitaji maalum 481 na walimu wenye ulemavu 176, mafundi sanifu na wahandisi 150 wameajiriwa.

Alisema serikali imeweka kipaumbele kuajiri walimu wa shule za sekondari zenye michepuo ya Sayansi na Hisabati, Ufundi, Kilimo na Biashara, Maarifa ya Nyumbani, lugha ya Kichina, Kiingereza na Kifaransa.

"Walimu wa masomo mengine wamepangwa katika vituo kulingana na upungufu uliopo, kwamba kipaumbele ni shule ambazo hazina kabisa walimu husika," alisema Mhandisi Nyamhanga.

Kadhalika, alisema kwa shule za msingi upangaji wa walimu umefanyika kwa lengo la kuboresha uwiano wa walimu, kwa wanafunzi na TAMISEMI imewapanga zaidi walimu hao katika shule za vijijini, ambako ndiko kwenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu.

Alifafanua kuwa walimu walioajiriwa kwa shule za msingi ni katika ngazi ya darasa la IIIA wenye Astashahada ya ualimu, daraja IIIB wenye Stashahada ya ualimu ya somo la Kiingereza na aliyesomea elimu ya awali.

"Pia Walimu wa daraja la IIIC wenye Shahada ya Ualimu kwa masomo ya Kiingereza, Uraia, Historia, Jiografia na Kiswahili ambao wapo 1,100 wameajiriwa na walimu wenye Daraja IIIB na IIIC waliohitimu Stashahada ya ualimu maalum kwa masomo ya lugha, Sanaa, sayansi na hisabati,"alisema Mhandisi Nyamhanga.

Hata hivyo, kwa upande wa ualimu shule za sekondari, Katibu Mkuu huyo alisema wameajiriwa katika makundi saba ambayo ni ualimu daraja la IIIB wenye Stashahada ya masomo ya Fizikia, Hisabati, Bailojia, Kemia, Uchumi na Sayansi ya Kilimo.

Pia alisema walimu wa daraja IIIC wenye shahada ya ualimu waliosomea masomo ya Sayansi ya Kilimo, Lugha ya Kiingereza, Lugha Sanifu ya Kiingereza, Kichina, Kifaransa, Utunzaji wa Hesabu, Biashara, Uhasibu na Uchumi.

"Wengine ni walimu wa Daraja la IIIB waliohitimu Stashahada ya ufundi, Daraja IIIC waliohitimu Shahada ya Uhandisi katika fani ya ujenzi, umeme na Mitambo na Mafundi Sanifu wa Maabara wahitimu wa Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara na Stashahada ya Sayansi na Teknolojia ya


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 84 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MELKIZEDECK PETER MSANGI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**DK. MICHAEL NATHAN NDAMO MSANGI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10th Mwezi wa Decemba, 2020.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10th Mwezi wa Novemba, 2020.

NAIBU MSAJILI

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 506 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**IVO MPINA MAYEKA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**NORGAITTY MAYEKA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10th Mwezi wa Decemba, 2020.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 9th Mwezi wa Novemba, 2020.

NAIBU MSAJILI

## Bilionea madini amtaja Magufuli

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MCHIMBAJI mdogo wa madini kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai, Gabriel Laiser, ambaye aliibuka bilionea baada ya kupata madini ya ruby yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.7, amemshukuru Rais John Magufuli kwa mafanikio aliyoyapata.

Laizer alipata madini hayo kupitia mgodi wake ulioko eneo la Mundarara, Longido mkoani Arusha mwishoni mwa wiki.

Akizungumza na waandishi wa habari, Laizer alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwapa kipaumbele wawekezaji wa madini wazawa, kusema kuwa bila yeye (Rais Magufuli) kusingekuwapo na Mtanzania ambaye angetajirika kutokana na madini.

Alisema mabilionea wa kizawa wamepatikana baada ya Rais magufuli kuingia madarakani, kuwapa kipaumbele wachimbaji wazawa hali iliyosababisha kupatikana kwa mabilionea, tofauti na miaka iliyopita.

"Nimshukuru Rais Magufuli maana kipindi cha nyuma Watanzania walikuwa hawapewi kipaumbele kuwekeza katika migodi, Ila yeye ameweza kuzuia wawekezaji kutoka nje ya nchi na sasa tangu wazawa waingie tumeweza kuona faida," alisema Laizer na kuongeza:

"Kwa sasa tunapata matajiri wapya wa madini, pia tunaona namna wazawa tulivyowazalendo kwa nchi yetu kwani hatutoroshi madini badala yake tukiyapata tunaitaarifu serikali ili waje waangalie, wapate mapato," alisema Laizer.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha nyuma wachimbaji wazawa walikuwa wakinyanyaswa na baadhi ya matajiri, lakini tangu uongozi wa Rais Magufuli uingie madarakani wamekuwa wakiishi kwa amani.

Aidha, aliwataka wachimbaji madini ambao wanatorosha madini kuacha tabia hiyo na kufuata njia ya haki na salama ya kulipa serikali.

Alieleza kuwa alipata tani tano za madini yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7, lakini bado ana ndoto za kufanya kazi kwa vifaa vya kisasa ili aweze kupata madini mengi zaidi.

Alifafanua kuwa katika mgodi wake ameajiri vijana zaidi ya 80 na kubainisha kuwa mgodi huo anaumiliki kwa asilimia mia.

Aidha, aliwasihi wachimbaji wenzake kuendelea kuchimba kisasa na kumuamini Mungu, ili wapate madini mengi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Muumini wa Dini ya Kiislam, baada ya kuhudhuria Sala ya Ijumaa katika Masjid Noor Muhammad jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Polisi waliofukuzwa kazi wadaiwa kuuawa katika tukio la ujambazi

**Na Romana Mallya**

ASKARI polisi wawili waliofukuzwa kazi kutokana na utovu wa nidhamu, wameuawa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kinondoni, baada ya kudaiwa kujihusisha na vitendo vya uhalifu wa kutumia silaha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna msaidizi (ACP) Ramadani Kingai, alisema watuhumiwa hao wa ujambazi waliuawa juzi eneo la Mbezi Luguruni baada ya kupata taarifa zao wakitaka kufanya uhalifu maeneo hayo.

Kingai aliwataja walioouawa ambao waliwahi kulitumikia jeshi la polisi kuwa ni XF 407 Koplo Bundala Said, maarufu Kimenya, ambaye alifukuzwa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi (RCO) wa Mkoa wa Kinondoni kwa matendo ya kihalifu. Mwingine ni XF 1205 Koplo Muhidini Sadiki, maarufu Mhina, ambaye alifukuzwa kazi akiwa Kituo cha Polisi cha Kimara kwa matendo ya uhalifu.

Akisimulia tukio hilo, Kamanda Kingai alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Kinondoni lilipata taarifa zao kuwa wamepanga kufanya uhalifu wa kutumia silaha eneo la Kiluvya.

"Kikosi maalum cha kupambana na majambazi kiliweka mtego eneo la Luguruni katika kituo cha mafuta kiitwacho Hapa Kazi Tu kilichoko karibu na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo. Watuhumiwa hawa walikuwa wakitokea eneo la Kimara kuelekea (kwenda) Kiluvya," alisema.

Baada ya watuhumiwa hao kufika Luguluni, alisema, wakiwa na gari lenye namba za usajili T 889 DKG aina ya Toyota Brevis lenye rangi ya Silver waliposimamishwa na polisi waligoma na kugeuza na kurudi walikotoka.

Alisema wakati askari wakiwafuatilia watuhumiwa hao ujambazi walianza kuwafyatulia polisi risasi na walipofika eneo la Mbezi Luis karibu na Shule ya St. Anne Maria, gari hilo lilipigwa risasi na kupoteza mwelekeo na kuingia mtaroni. "Katika tukio hili mtuhumiwa wa ujambazi mmoja aliuawa papo hapo na watatu walikimbia huku mmoja wao akiwa na jeraha mguuni," alisema.

Kamanda Kingai alisema baada ya muda kupita, Jeshi la Polisi lilipata taarifa kuwa miongoni mwa watuhumiwa hao ameonekana eneo la Ubungo Kibo katika kituo cha daladala akitaka kupanda gari.

"Askari walifika eneo hilo na alipowaona alijaribu kukimbia huku akirusha risasi lakini polisi walimkamata.

Tunaendelea kuwasaka wenzao wawili waliokuwa pamoja. Katika eneo la tukio kulikutwa maganda manne ya risasi," alisema.

# Kiboko, mkewe wana kesi ya kujibu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi, imesema washtakiwa Ayubu Kiboko na mke wake, Pili Kiboko, wana kesi ya kujibu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Lilian Mashaka, baada ya kusikiliza mashahidi sita wa Jamhuri.

Jaji Mashaka alisema kutokana na ushahidi uliotolewa na mashahidi hao wa Jamhuri, bila kuacha shaka, mahakama yake imeona kwamba wana kesi ya kujibu.

"Mahakama bila kuacha shaka, imeona washtakiwa wote wawili mna kesi ya kujibu. Mtapanda kizimbani kujitetea Novemba 30, mwaka huu," alisema Jaji Mashaka.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali, Omary Msemo, Constantine Kakula na Kanditi Nasua, ulidai kuwa unafunga kesi yao baada ya kuita mashahidi sita na vielelezo 16 kuthibitisha makosa dhidi ya washtakiwa.

Washtakiwa kwa nyakati tofauti walidai mahakamani kwamba watajitetea wenyewe hawatakuwa na shahidi chini ya kiapo.

Msemo alidai upande wa Jamhuri unaomba magari matatu kati ya waliyoyakamata yawe chini ya Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA).

Jaji Mashaka alikubali ombi la Jamhuri na alikabidhi vielelezo hivyo vilivyopewa namba 13, 14 na 15 (magari) kwa Inspekta Hassan Msangi kwa ajili ya kuhifadhi na kwamba ayawasilishe mahakamani Jumatatu ijayo.

.Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Mei 23, 2018 katika eneo la Tegeta Nyuki Wilaya ya Kinondoni, washtakiwa walikuwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroine gramu 251.25.

# Mvua yaacha simanzi jijini Mwanza

**Na Richard Makore, MWANZA**

MVUA kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia jana katika maeneo mengi jijini Mwanza, imeacha vilio katika badhi ya maeneo baada ya nyumba kujaa maji na wananchi kupoteza mali zao.

Mafuriko hayo yalitokea baada ya mvua kubwa yenye upepo kunyesha mfululizo kwa takribani saa mbili, hivyo kuleta madhara kwa baadhi ya maeneo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyamanoro A, Fredy Maregesi, alisema baadhi ya nyumba kuta zake zimeanguka na kwamba samani za ndani nyingi zimeharibika.

Kutokana na maafa hayo, mwenyekiti huyo aliomba serikali kurekebisha miundombinu ya barabara na mitaro ili kuwanusuru wananchi.

Aliongeza kuwa miundombinu mingi ni mibovu na midogo na kwamba mtaa wake una kaya 550 na kati ya hizo, 80 zimekumbwa na mafuriko.

Naye Diwani Mteule wa Nyamanoro, George Maganiko, alisema makalavati yako tofauti na mitaro hatua ambayo inasababisha kuwapo na mafuriko.

Alisema maeneo mengine kwa sasa yameziba na kuahidi kwamba akishakula kiapo cha udiwani, atafuatilia ili kuhakikisha miundombinu inakuwa sawa ili kuondoa mafuriko hayo ambayo hutokea mara kwa mara.

Alisema wakazi wengi wanajenga bila kufuata utaratibu na kwamba baadhi yao wanatupa takataka ambazo huziba mitaro na hivyo kusababisha mafuriko.

Rosemary Ngonyani, mkazi wa mtaa wa Nyamanoro A, aliomba serikali kuwaangalia ikiwamo kuwajengea miundombinu imara inayoweza kubeba maji wakati wa mvua.

Alisema miaka ya nyuma hali haikuwa kama ilivyo sasa ya kutokea mafuriko na kwamba mvua iliyoanza kunyesha saa nane usiku wa kuamkia jana, imewasababishia hasara ikiwamo kuharibika vitu vya ndani.

Akizungumzia sakata hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema mpaka jana mchana alikuwa hajapata taarifa za vifo vya watu.

Kamanda Muliro alisema maeneo mbalimbali ya jiji yalikumbwa na mvua kubwa usiku wa kuamkia jana, lakini hajapokea matukio ya watu kupoteza maisha.



Mbunge wa Viti Maalum kupitia Jumuiya ya Wazazi ya CCM, Bahati Keneth (kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha watoto yatima cha Buloma, wilayani Kibaha, mkoani Pwani juzi. **PICA: JUMANNE JUMA**

# Mpango aahidi ufumbuzi soko la tangawizi

**Na Mwandishi Wetu, KIGOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameahidi kulipatia ufumbuzi tatizo la soko la Tangawizi linalozalishwa kwa wingi katika Kata ya Munzeze, Buhigwe mkoani hapa.

Mpango ametoa ahadi hiyo juzi, akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani hapa akiahidi kwamba atatafuta masoko ndani na nje ya nchi ili wananchi wafaidike na kilimo cha zao hilo la biashara ambalo ni chanzo kikubwa cha kipato.

"Nikiwa kwenye kampeni wakati wa uchaguzi mkuu, nilishuhudia wafanyabiashara kutoka nchini Burundi wakinunua tangawizi mbichi kwa bei ya chini na kuipeleka nchini mwao na kuichakata kisha kutuletea hapa nchini na kutuuzia kwa bei ya juu. Hili halikubaliki, sisi tunatakiwa kuongeza thamani ya tangawizi na kuiuza nchini mwao" alisema.

Sambamba na hilo, Dk. Mpango aliwaahidi wananchi hao kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa vya Shule ya Sekondari Kigogwe inayojengwa kwa nguvu za wananchi ili kuboresha elimu katika kata hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Kanali Michael Ngayalina, alisema wilaya yake inakabiliwa na umasikini kwa wananchi wake na kumwomba Waziri Mpango ambaye pia ni Mbunge wa Buhigwe, kuwasaidia kuondokana na hali hiyo kwa kuimarisha sekta ya kilimo.

Alisema bei ya tangawizi inamsononesha kwa kuwa wananchi, hususan wa Kata ya Munzeze ambao ni wakulima wazuri wa zao hilo, wanauza kilo moja ya zao hilo kwa kati ya Sh. 400 na 700, bei ambayo alisema ni ndogo na haiwanufaishi wakulima.

"Nimeingia kwenye mitandao kutafuta mashine za kuongeza thamani ya tangawizi. Nimeona kuna mashine za kuosha Tangawizi, kuchambua, kuchakata na kufungasha zao hilo na zana hizi zikipatikana, wananchi wa Munzeze wataondokana na kuuza kwa kwa bei ya hasara," alisema Kanali Ngayalina.

Naye Diwani wa Munzeze, Wilson Vyabhoze, alimwomba Waziri wa Fedha na Mipango, kuona namna ya kuanzisha taasisi ambazo zitakuwa zinauza mbegu za mazao mbalimbali ikiwamo tangawizi ili kuwarahisishia wananchi upatikanaji wake kwa kuwa ardhi yao ina rutuba ya kutosha.

Katika ziara hiyo, Dk. Mpango ametembelea pia Kata ya Janda, ambako wananchi wa eneo hilo waliomba atatue tatizo la zahanati na kuahidi kushughulikia kwa haraka jambo hilo.

Pia alitembelea Kata ya Bukuba na aliahidi kumalizia ujenzi wa zahanati mbili ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi hadi hatua ya renta kwa ajili ya kuhudumia vijiji vya Bukuba na Kibuye.

# Serikali yaokoa trilioni 33/- gesi

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

SERIKALI imeokoa Sh. trilioni 33 kutokana na matumizi ya gesi asilia, badala yake imezielekeza katika matumizi mengine katika kukuza uchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio, alisema hayo jana katika mkutano mkuu wa mwaka wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania, uliofanyika jijini hapa.

"Tumeokoa Sh. trilioni 33 kutokana na matumizi ya gesi asilia na kuielekeza kwenye matumizi mengine. Lakini pia tumelipa takribani Sh. bilioni 600 kodi mbalimbali kutokana na mauzo ya gesi asilia," alisema.

Dk. Mataragio alisema TPDC imerejea katika biashara ya mafuta na bidhaa zake kupitia kampuni tanzu ya TANOIL ambayo iliundwa na TPDC kwa mujibu wa sheria, lengo likiwa kuendesha biashara hiyo.

Pia alisema sasa TPDC imetwaa maeneo kadhaa nchini ikiwamo katika mikoa ya Tanga, Dodoma na Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga maghala ya kuhifadhia mafuta ya kimkakati.

Alisema ndani ya miaka mitano ijayo, serikali inatarajia kujenga vituo vya mafuta 100 nchi nzima kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali na sekta binafsi.

Mkurugenzi mtendaji huyo alisema mafanikio hayo yote yataifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha kuhudumia nchi za Afrika Mashariki na Kati na kukuza uchumi wa viwanda vya ndani, kuongeza fursa za ajira na kuchangia pato la taifa.

Alisema hivi sasa wamepokea maombi kadhaa kutoka nchi jirani za Zambia, Kenya na Uganda kutokana na uhitaji wa malighafi hiyo ya gesi asilia.

Kwa mujibu wa Dk. Mataragio, TPDC imejitangaza na kujipambanua vizuri kwa wadau wake, hivyo inatambua katika kufikia malengo iliyojiwekea kwenye utafutaji wa mafuta na gesi ikishirikiana na wajiolojia.

**"Tumeokoa Sh. trilioni 33 kutokana na matumizi ya gesi asilia na kuzielekeza kwenye matumizi mengine. Lakini pia tumelipa takribani Sh. bilioni 600 kodi mbalimbali kutokana na mauzo ya gesi asilia," alisema.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba SC, Namungo michuano CAF

**MASHINDANO** ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ambayo yanaandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF),yanatarajiwa kufanyika katika viwanja mbalimbali kuanzia leo barani hapa.

Michuano hiyo inashirikisha mabingwa wa Ligi Kuu za nchi wanachama pamoja na klabu nyingine zilizofanya vyema kwenye ligi hizo na mabingwa wa Kombe la FA.

Kwa upande wa Tanzania Bara katika mashindano hayo kwa mwaka huu, wawakilishi wake ni Simba ya jijini, Dar es Salaam ambayo itashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Namungo ya Lindi itakayopeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba yenyewe itaanza kuwania taji hilo la ubingwa wa Afrika ugenini Nigeria dhidi ya Plateau United, mechi itakayofanyika kesho Jumapili kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki wakati Namungo FC yenyewe itawakaribisha Al Rabita FC kutoka Sudan Kusini leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam.

Wawakilishi wengine wa nchi katika michuano hiyo kutoka Zanzibar ni Mlandege watakaowakaribisha CX Safien ya Tunisia katika mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa itakayochezwa leo wakati KVZ yenyewe ikiwa ugenini Sudan kuvaana na wenyeji wao El Amal kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho.

Simba na Namungo zinakwenda katika mashindano hayo zikiwa zimefanya maandalizi yake kupitia mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo hadi wanaingia kwenye michuano hiyo, wamecheza michezo 10.

Nipashe inaamini makocha wa timu zote, watakuwa wamerekebisha makosa waliyoyabaini kwenye mechi za ligi ili yasijirudie watakapokuwa wanapeperusha bendera ya nchi katika michuano hiyo ya kimataifa.

Kila timu hizo zinaposhuka uwanjani, zitanakiwa kukumbuka hawawakilishi wanachama au mashabiki wao tu, bali wanawakilisha jina la Tanzania ambayo inaongozwa na Rais Dk. John Pombe Magufuli, hivyo watatakiwa kupambana kwa dakika zote 90 watakazokuwa uwanjani.

Katika mpira hakuna miujiza, timu ambayo itakuwa imesajili vizuri, imejiandaa vyema na itakayotumia kwa umakini nafasi za kufunga ilizotengeneza, itakuwa imejiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele. Tanzania haikuwa na matokeo mazuri katika mashindano hayo ya CAF msimu uliopita, baada ya timu zake, nne kutoka Bara na mbili za Zanzibar zilizokuwa zinapeperusha bendera kushindwa kufika kwenye hatua ya makundi, na kuipoteza nafasi ya kutoa klabu nne katika michuano hiyo msimu huu.

Matokeo mazuri yanatokana na maandalizi sahihi, Nipashe inaamini Simba, Namungo, KVZ na Mlandege zilitumia muda wa maandalizi kwa ya Ligi Kuu wanazoshiriki, sambamba na kujiweka tayari kupambana kwenye mashindano hayo ya kimataifa.


Inafahamika wazi, timu itakayocheza soka la kiwango cha juu, ndio itavuna matokeo chanya kwa sababu huwezi kushinda mechi yoyote ya mpira wa miguu au mchezo wowote dunaini kama hukufanya maandalizi mazuri.

Pia tunawakumbusha wadau wa michezo nchini kuwapa ushirikiano wawakilishi wetu, hasa pale watakapokuwa wanacheza mechi za nyumbani kwa kuwashangilia na kuwaombea dua njema kwenye mapambano yao.

Ni wazi timu zote hazikupata muda wa kutosha wa maandalizi kabla ya msimu 'pre-season', lakini hili lisiwe kigezo cha wao kwenda kufanya vibaya katika mashindano hayo ya kimataifa, wachezaji nendeni mkapambane kwa ajili ya timu zenu, taifa lenu, lakini vile vile kutangaza vipaji vyenu kwa mawakala wa kimataifa.

**Mungu ibariki Simba SC, Namungo FC, Mlandege FC na KVZ FC, Mungu ibariki Tanzania.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Watani wa jadi hawakomoani

**TOLEO** lililopita la gazeti hili niliandika makala inayozihusu timu za Simba na Yanga yenye kichwa: "Umbea wa Simba, Yanga."

Msomaji aliyesoma makala yangu alinitumia ujumbe wa simu akiniambia: "Uliyoandika ni maoni yako ila Simba na Yanga ni 'watani wa jadi' na si 'wapinzani wa jadi' kama ulivyoandika."

Kama alivyosema kuwa 'wapinzani wa jadi ni maoni yangu,' nakubaliana naye kwa asilimia 100. Nami namwambia 'watani wa jadi ni maoni yake.' Naomba sasa nimzindue kwa kumwelewesha tofauti ya 'watani' na 'wapinzani.'

Kwa mujibu wa Kamusi Kamili la Kiswahili, 'utani' ni taratibu au desturi za kimila ambazo zinawafanya watu wanaojuana kuambiana au kutendeana jambo lolote bila kuleta chuki au kero; maneno ya kutania; dhihaka, masihara.

Kwa hiyo 'upinzani' ni hali au tendo la kupinga; ukinzani. Kundi au upande unaopinga uongozi au chama kinachotawala.

'Utani' ni taratibu za kimila zinazowafanya watu kuambiana au kutendeana jambo lolote bila chuki. Maneno ya kutania; dhihaka, masihara, kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

Kamusi ya Karne ya 21 yaeleza maana ya 'utani' kuwa ni taratibu au desturi za kimila zinazowafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila chuki au kero; maneno ya masihara/maskhara; dhihaka.

'Upinzani' ni hali au tendo la kupinga; ukinzani. Kundi au upande unaopinga uongozi au chama kinachotawala.'Utani' ni maneno au vitendo vya dhihaka; mzaha. Tabia ya watu kufanyiana masihara/maskhara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha.

Kamusi ya Visawe (maneno ambayo maana yake hufanana na kukaribiana kimaana na maneno mengine; sinonimu) yaeleza maana ya 'utani' kuwa ni dhihaka, masikhara/masihara, mzaha, mchezo, stihizai, saguo, shere, kejeli, tashtiti, chuni, goya, mayaza, utiriri, ufyosi, chati, kichekesho, maneno ya kutaniana. 'Upinzani' umeelezwa kuwa ni ukinzani, ubishi, ushindani, mvutano, mghalaba. Kutokana na visa vifanywavyo na timu za Yanga na Simba ambazo mwaka 1935 zilikuwa moja kabla ya kufarakana mwaka 1936, nashindwa kukubaliana na kile kisemwacho eti timu hizo ni 'watani wa jadi.' Badala yake nimekuwa nikiziita 'wapinzani wa jadi'.

Maana ya jadi ni asili ya mtu kama vile uzawa, ukoo au nasaba; mwenendo wa mtu; mambo ya asili ambayo watu wa kabila fulani hurithi kutoka kwa mababu zao;

Hizo ndizo sababu zinazonifanya kuzipa Yanga na Simba jina la 'wapinzani wa jadi' badala ya 'watani wa jadi.' Sababu hizo nimeziorodhesha huko juu kwa kueleza tafauti/tofauti za 'wapinzani' na 'watani.'

Namwuliza aliyenitumia ujumbe kukanusha kuwa Yanga na Simba si 'wapinzani wa jadi' bali ni 'watani wa jadi.' Je, watu wanaotengana huitwaje 'watani' ilhali hawana uhusiano waliokuwa nao kabla?

'Watani wa jadi' huchekana upande mmoja unaposhambuliwa na adui? Kwa nini timu yoyote kati ya hizo ziitwazo 'watani wa jadi' hushangilia sana wakati ingine ikifungwa na timu ngeni inayotoka nje ya Tanzania?

Mbona timu hizo hudhuriana na kuchukuliana wachezaji kwa hila na kutambiana? Huo ni utani au uadui? Nijuavyo ni kwamba watani hawagombani wala kufanyiana uhasama upande mmoja unapopatwa na matatizo, bali hutaniana tu huku wakisaidiana kwa dhati.

Ukitaka kuthibitisha, nenda msibani uone jinsi familia iliyofiwa inavyosaidiwa na watani wao wa jadi. Sehemu kubwa ya kazi zifanywazo nyumbani hufanywa na Watani wa jadi. Kwa wafiwa, watani wa jadi hupita na sahani kuomba mchango wa fedha kwa waombolezaji waliofika kilioni. Wengine hujaribu hata kuigiza sauti na mwendo wa marehemu!

Wanaofuatilia kabumbu la Ligi Kuu msimu huu wataona timu zinazoshiriki zina wachezaji hodari na shupavu kiasi cha kushangaza hata kujiuliza: "Kwa nini Simba na Yanga hutumia mamilioni ya fedha kusajili wachezaji wa kigeni ilhali Tanzania ina wachezaji wengi wazuri na shupavu zaidi yao?"b "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Methali hii yatufunza tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine.

'Taamuli' ni uwezo wa kuzingatia jambo; tafakuri. Kitendo cha kutia jambo akilini; zingatia.

**Kazi kwenu wasomaji.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Mbunge wa Handeni Mjini, mkoani Tanga, Kwagilwa Reuben, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiishauri serikali kuhusu njia bora ya kudhibiti mfumko wa bei ya saruji nchini, ikiwa ni pamoja na viwanda kuongeza uzalishaji kulingana na mikataba yao ya uwekezaji. Kushoto ni Mwananchi, Hussein Sheng'wamkai. **PICHA: JOHN BADI**

# Ndugai ataja mwarobaini tatizo la ajira

**Na Christina Mwakangale**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema njia kubwa ya kumaliza tatizo la ajira miongoni mwa vijana ni kujiajiri kupitia elimu wanayoipata katika taasisi za elimu ya juu.

Amesema itaondoa dhana iliyopo katika jamii kuwa uwekezaji kwenye elimu unaofanywa na serikali na wadau wake si kitu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika mahafali ya 46 ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Ndugai alisema lazima iwepo tofauti kati ya mtu alihitimu elimu ya msingi hadi chuo.

"Mjadala mkubwa bungeni ni kumsomesha mtoto hadi elimu ya juu, kuanzia shule ya msingi, sekondari hadi chuo. Mzazi anahoji uwekezaji wote huu wa nini?," alisema Ndugai na kuongeza:

"Wazazi wanaulizana kwa sababu wasomi wetu mmejazwa na kujijaza ujuzi, hamjiajiri mnasubiri kuajiriwa. Sekta elimu inazungumzwa ijadiliwe upya ili kufahamu kilicho bora," alisema Ndugai.

Alisema ndani ya jamii walio na elimu ya darasa la saba ndiyo huwaajiri wenye shahada, huku walio na utajiri wakiwa na elimu ya kawaida.

"Kuna usimamizi wa fedha unahitajika katika ufugaji, kilimo. Badala ya mhitimu unakaa nyumbani kuangalia televisheni kutwa au kushinda mtandaoni," alisema Ndugai.

Kadhalika, alisema vijana wanapaswa kujiamini Katika kuanzisha biashara huku akiwakumbusha wahitimu hao kuanza kulipa fedha ya mkopo wa elimu ya juu, ili kunufaisha wahitaji wengine.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Thadeus Satta, alisema wahitimu wa mwaka huu, 3,962 wametunukiwa vyeti kampasi ya jijini Dar es Salaam na kwamba kuna ongezeko la udahili wa wanafunzi tangu chuo kuanzishwa mwaka 1972.

Alisema chuo kilipoanzishwa wanafunzi 72 walidahiliwa, huku mahitaji yakiongezeka hivi sasa, kwamba tangu mwaka 1972 hadi mwaka wa masomo 2019/20 walihitimu ni 12,565 na idadi ya kozi zinazofundishwa ni 34.

Prof. Satta alisema zipo kero mbalimbali zinazowakabili mojawapo ni idadi ndogo ya wakufunzi na uwiano wa wahadhiri kufundisha.

# Wanawake watonywa fursa za kidigitali

**Na Romana Mallya**

WAFANYABIASHARA wanawake wametakiwa kuchangamkia fursa za kidigitali kwa ajili ya kuboresha biashara zao, pamoja na kuwa wabunifu.

Rai hiyo ilitolewa jana katika mkutano uliowakutanisha wadau wa digitali, ulioandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Wafanyabiashara wa Norway (NHO), kupitia Umoja wa Wahitimu wa Programu ya Wanawake Kiongozi (FFAT)

Mkurugenzi Mkazi wa TradeMark East Africa Tawi la Tanzania, John Ulanga, alisema wanawake wana nafasi ya kufikia mafanikio waliojiwekea kwa kutumia fursa ya kidigitali, kwa sababu huko ndiko dunia iliko kwa sasa.

Mshauri wa Mawasiliano ya Kidigitali na Mkurugenzi wa kampuni ya KEM Solutions, Kai Mollel, alisema mitandao ya kijamii ina fursa kubwa ambazo bado hazijatumiwa kikamilifu.

"Siku hizi wanawake wengi hutumia muda mwingi kwenye mitandao bila kufanya chochote cha kuwaingizia kipato, wanatumia muda mwingi kwenye simu kutafuta vitu mitandaoni ambavyo havina matokeo chanja kwao.

Baadhi yao hawajui umuhimu wa uchumi wa mitandaoni," alisema Mollel.

Mollel alisisitiza umuhimu wa programu za kuwajengea uwezo wa kutambua fursa za utajiri zinazopatikana mitandaoni.

Aliwahimiza wanawake kutumia fursa za kidigitali katika sekta mbalimbali kwa masuala ya usawa wa kijinsia, ili kuongeza uvumbuzi na kuleta faida za kuchumi kwao na kwa nchi.

Mshauri wa Kimataifa kuhusu masuala ya Teknolojia Habari na Mawasiliano, mageuzi ya viwanda na uchumi kimtandao, Mhandisi Peter Ulanga, ambaye pia ni mstaafu wa Taasisi ya Kimataifa ya mawasiliano, alisema wanawake katika kufanikiwa kidigitali wanatakiwa kutengeneza mawazo yao yenye mtazamo mzuri.

"Tunapotumia fursa za kidigitali tunatakiwa kukumbuka kulinda taarifa na faragha, hili ni eneo lingine ambalo linahitaji kuchukuliwa hatua zaidi kusaidia wafanyabiashara wanawake ili kuwawezesha kubaki salama na kufaidika na uchumi wa kimtandao," alisema Ulanga.

Mratibu wa masuala yanayohusu wanawake kutoka ATE, Anabahati Mlay, alisema kauli mbiu isemayo, 'Kuwaleta pamoja wanawake wenye vipaji kwenye uchumi wa kidigitali' imewaleta pamoja wanawake kutoka taasisi binafsi na za umma kujadiliana na kupeana uzoefu ili kusaidia kutimiza ndoto zao kwa kutumia teknolojia.

# RC awapa somo mabalozi utalii

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amewataka mabalozi 13 wa utalii kutoka mikoa Kagera, Geita na Kigoma kutangaza sekta hiyo kimataifa.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akizungumza na Mamisi Utalii Kanda ya Magharibi kwa mwaka 2020, waliofika ofisini kwa lengo la kujitambulisha.

"Nyie msiishie hapa kuweni mabalozi wa utalii ndani na nje ya nchi na popote mtakapofika kulitangaza nchi yetu watu wafike kwa wingi,'' alisema Gaguti

Mkurugenzi wa Grace Entertainment, Grace Shija, alisema uwepo wa mashindano hayo ni kutaka Kanda ya Magharibi iwe na utalii sawa na maeneo mengine.

# Airlink kuanza Safari Afrika Kusini Desemba

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Ndege la Airlink linatarajia kuzindua safari za ndege kutoka Tanzania kwenda Afrika Kusini, Desemba Mosi, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo, Rodger Foster, alisema: "Airlink inaendelea kuboresha huduma zake, njia mpya ya ndege kutoka Jiji la Dar es Salaam hadi Johannesburg Afrika Kusini itaongeza undugu katika uchumi, kisiasa na kibiashara. Kwa sasa tunaandaa kutafuta wakala wa mauzo atakayetuwakilisha Tanzania."

Alisema kuanza kwa safari hiyo pia kumefungua safari zingine katika miji ya Port Elizabeth, East London, Bloemfontein na kwamba Airlink inaendelea kujitanua katika nchi zingine za SADC.

Pia alisema katika daraja la uchumi wa kati abiria ataingia na mzigo wa kilo 20 bure na ndani ya ndege kunatolewa huduma za viburudisho na chakula.

Airlink ni shirika linalotoa huduma za usafiri wa ndege kimataifa.

# Wahamiaji haramu 52 wanaswa Mwanza

**Na Richard Makore,** MWANZA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Mwanza inawashikilia watu 52 raia wa Ethiopia waliokamatwa katika nyumba moja eneo la Buhuku, wilayani Nyamagana kwa tuhuma za kuishi nchini bila kibali. Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza, Bahati Mwaifuge, alisema wahamiaji hao walikutwa wamehifadhiwa katika nyumba hiyo ambayo haikaliwi na wenyeji.

Mwauifuge alisema baada ya mahojiano, wahamiaji hao walikiri kuingia nchini bila kufuata utaratibu na kwamba lengo lao lilikuwa kwenda Afrika Kusini kutafuta maisha.

Alisema kati ya wahamiaji hao haramu, wanne walikamatiwa nyumba ya kulala wageni iliyoko eneo la Mabatini jijini Mwanza na wengine 48 walikutwa Buhongwa.

Ofisa huyo alisema kumekuwa na wimbi kubwa la wahamiaji haramu kuingia nchini na kwamba kwa mwezi huu pekee, idadi hiyo inafikia 59 kwa kuwa saba walishakamatwa na kesi zao ziko mahakamani.

Mwaifuge alisema kazi hiyo waliifanya kwa kushirikiana na jeshi la polisi na kwamba baada ya taratibu kukamilika watafikisha mahakamani.

Aliongeza kuwa kosa la kuingia nchini kwa njia haramu, adhabu yake ni kifungo cha miaka 20 jela na faini ya Sh. milioni 20.

Aliwataka wakazi wa Mwanza kukataa kupokea na kuwahifadhi wahamiaji kutoka nchi yoyote kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria, badala yake wakiwaona watu wa namna hiyo, watoe taarifa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.



Mafundi wakipiga plasta moja ya majengo ya Kituo cha Afya cha Kata ya Bugwema Wilaya ya Musoma mkoani Mara juzi, ambacho kinajengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Chanzo cha utapiamlo, upungufu damu kwa wajawazito chatajwa

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

UKOSEFU wa elimu ya uandaaji wa chakula chenye lishe katika Kijiji cha Wishiteleja Kata ya Mondo, Kishapu mkoani Shinyanga, umesababisha kuwapo kwa watoto wenye utapiamlo na upungufu wa damu kwa wajawazito.

Aidha, imeelezwa kuwa mila na desturi potofu kwa baadhi ya jamii zimekuwa zikimkandamiza mwanamke mjamzito kwa kumnyima vyakula vyenye lishe.

Kauli hiyo ilitolewa jana katika kijiji cha Wishiteleja na Mratibu wa Lishe mkoani Shinyanga, Denis Madeleke, wakati wa ufuatiliaji wa mradi wa uboreshaji huduma za lishe.

Alisema mradi wa ufuatiliaji wa lishe unatekelezwa katika halmashauri tano za mikoa ya Shinyanga na Singida chini ya shirika la World Vision Tanzania kwa ufadhili wa serikali ya Canada.

Mratibu huyo alisema Kijiji cha Wishiteleja kina watoto 190 wenye umri kuanzia miezi sita hadi miaka miwili na kati ya hao 71 walifanyiwa tathmini na kubaini watoto 22 wakiwa na utapiamlo.

Madeleke alisema ukuaji wa mtoto unaanzia wakati mimba inapotungwa hadi siku 1,000 na kwamba akikosa lishe bora atakuwa na udumavu maisha yake yote.

Alisema kabla ya utekelezaji wa mradi huo hali ya utapiamlo mkoani Shinyanga ulikuwa na asilimia 59 kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 lakini kwa sasa umepungua hadi asilimia 30.4 kwa mwaka 2018, udumavu asilimia 30.2 na ukondefu asilimia nne.

Mratibu wa mradi huo, Frank Mtimbwa, alisema walianza kutekeleza tangu mwaka 2016 katika halmashauri tano za mikoa ya Shinyanga na Singida na unatarajia kukamilika machi 2021.

Alisema lengo la utekelezaji wa mradi huo ni kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wadogo chini ya miaka mitano.

## Tanzania yapania kuongoza uzalishaji wa mpunga Afrika

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKATI Tanzania ikiwa nchi ya pili kwa uzalishaji wa mpunga Afrika, imeanza kujipanga kwa kuweka mikakati mbalimbali ili ishike nafasi ya kwanza, ambayo inashikiliwa na Madagascar.

Ili kufanikisha lengo hilo, Shirika la Umoja wa Mataifa linalishughulikia Chakula (FAO) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, limeanza kuwajengea uwezo watafiti na wataalamu wa kilimo cha mpunga nchini kwa lengo la kuongeza mbinu za uzalishaji na kuhifadhi mpunga unaopotea baada ya mavuno.

Akifungua mafunzo ya awamu ya pili ya mradi wa uzalishaji wa mpunga na kuongeza thamani ya zao hilo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kolobelo, alisema mradi huo wa kuwajengea uwezo watafiti na wataalamu wa mpunga utafanyika katika wilaya za Kilombero na Mvomero.

Mhandisi Kolobelo alisema kuwapo kwa mradi huo kumetokana na awamu ya kwanza ulioanza 2016 ambao ulilenga kuongeza uzalishaji wa mpunga na kuleta matokeo chanya kwa mkoa wa Morogoro kwenye uzalishaji wa mpunga.

Alizitaja mafanikio hayo ni kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 2.5 kwa hekta na kufikia tani 5 kwa hekta, na kwa mkoa kutoka tani 500,000 hadi 800,000 za mpunga kwa mwaka baada ya kuwapo kwa mradi huo.

Alisema baada ya mradi huo kumalizika na kuleta mafanikio kupitia wahisani wa nchi za Venezuela na Korea Kaskazini waliomba kuongezewa kwa awamu nyingine ya pili na washirika waliona matokeo mazuri, hivyo walikubaliana na Serikali ya Tanzania.

Alisema kupitia mradi huo mpya, FAO na Serikali wamekuja na mradi huo mpya wa kuongeza uzalishaji na kuangalia namna ya kupunguza upotevu wa mazao kabla ya kuvunwa ili wananchi wazalishe kwa wingi na kushika nafasi ya kwanza kwa mpunga Afrika.

Mwakilishi Msaidizi wa FAO Tanzania anayeshughulikia miradi huo, Charles Tulahi, alisema mradi huo utahusisha nchi tatu zikiwamo Tanzania, Ivory Coast na Ufilipino kwa kuwajengea uwezo watafiti waweze kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mpunga.

Alisema mradi huo unatarajia kugharimu kiasi cha Sh. bilioni 2.3 kwa nchi hizo tatu na kwa Tanzania utafanyika katika Kituo vya Utafiti wa Kilimo Mpunga cha Dakawa kilichopo Mvomero na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Ifakala wilayani Kilombero vyote mkoani Morogoro.





Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Tunu Pinda, akifungua kongamano la kitaifa la wanawake wajasiriamali kutoka makanisa mbalimbali kuhusu mafunzo ya ujasiriamali jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri 45 zawekwa kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI za wilaya 45 zimepewa siku tano kujieleza sababu ya kutounda kamati za watu wenye ulemavu.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa wadau wa Chama cha Wazazi wa Watoto wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi.

Alisema hadi sasa halmashauri 140 zimeunda kamati hizo lakini zingine bado hazijafanya hivyo, jambo ambalo linarudisha nyuma mikakati ya serikali ya kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Dk. Gwajima alisema kamati hizo ni muhimu kuundwa kwa kuwa zinarahisisha mawasiliano kati ya jamii ya watu wenye ulemavu na serikali na kuweka mikakati bora ya jinsi ya kutatua kero zinazowakabili jamii kwa haraka.

"Kwa Halmashauri ambazo hazijaunda kamati hizo natoa siku tano kutoa maelezo wanataka nini ili waunde kamati hizo. Waliambiwa mwaka gani na sababu za kutokuunda kamati ni nini na wana mikakati gani ya kuanzisha kamati hizo?"alihoji.

Dk. Gwajima alisema kutokuundwa kwa kamati hizo kumesababisha kukata mawasiliano kati ya jamii ya watu wenye ulemavu na serikali katika utoaji wa huduma za afya kwa jamii. Kadhalika, aliwataka wadau mbalimbali nchini kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora kabla ya ujauzito ili kupunguza tatizo la watoto wenye mgongo wazi na vichwa vikubwa nchini.

"Kuna umuhimu wa kuweka mikakati itakayosaidia kutoa elimu kuanzia ngazi ya chini ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa jamii, itasaidia kumaliza au kupunguza kabisa tatizo la kupata watoto wenye vichwa vikubwa na migongo wazi," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuboresha huduma kwa kujenga na kukarabati vituo vya afya nchini na kupeleka vifaa tiba ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Katika hatua nyingine, Dk. Gwajima aliitaka jamii kuacha mila potofu za kuamini kuwa mtoto anapozaliwa na tatizo la mgongo wazi na kichwa kikubwa kuwa wamelogwa hivyo baadhi ya wazazi kuwaficha watoto wao jambo ambalo linawachelewesha kwenye matibabu.

Pia aliagiza wadau wote kuhakikisha wanatoa elimu kwa kamati za vituo vya afya nchini ili kujua takwimu sahihi ya watoto wenye vichwa vikubwa.

# Waandishi waonywa lugha za matusi, kashfa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuepuka kutumia lugha ya kashfa, uongo na uchochezi katika kuandika za habari za Bunge.

Vile vile, wametakiwa kutoandika habari kishabiki bila ya kusikiliza na upande wa pili.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbasi aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa mada katika semina ya waandishi wa habari wanaoandika habari za Bunge, iliyofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia kwenye uandishi wao.

Alisema baadhi ya waandishi wamekuwa wakikashfu au kutumia lugha ya kuudhi wabunge au bunge jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa vifungu vya 35, 50 na 52 vya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016. "Hata kama humkubali mtu kuna namna yake ya kusema si kuanza kumkashifu, kumtolea lugha ya kashfa. Hilo ni kosa mnapaswa kuepukana nalo.

"Kuweni makini na matumizi ya lugha, kupotosha lugha au kuwaita wabunge majina ambayo yanawadhalilisha kwa jinsia zao, dini zao, kabila lao. Linaweza kuwa kosa la dharau kwa Bunge," alisisitiza.

Dk.Abbasi ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, alisema mara kadhaa waandishi wamekuwa wakikosea kwa kuandika hoja ya mbunge mmoja kabla ya majibu ya waziri, serikali au mbunge mwingine. "Kwenye hili mwandishi pia usitumie hoja ya mbunge kuwa ndiyo ya bunge, unapaswa kusema hayo ni maoni ya mbunge na siyo kusema maoni ya bunge," alisema.

Aliwasisitiza waandishi kuwapa fursa wabunge wote kwa kuzingatia vyanzo vya habari kama wabunge wanawake wanapotoa hoja zao, wabunge wanaowakilisha makundi mengine ya kijamii mfano walemavu na wafanyakazi.

Awali, akifungua semina hiyo ya uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika habari za bunge kwa niaba ya Katibu wa Bunge, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa wa Bunge, Daniel Eliufoo, alisema semina hiyo imeandaliwa ili kuwajengea uwezo waandishi wa habari wa ripoti taarifa za kibunge kwa usahihi.

Naye Mratibu wa Mradi wa kulijengea uwezo Bunge unaofadhiliwa na UNDP, Angelus Turuka, alisema lengo la mradi huo ni kuliwezesha bunge kutekeleza majukumu yake vizuri. Alibainisha kuwa pia una lengo la kuwapa elimu waandishi wa habari namna bora ya kuripoti taarifa za bunge na kuwa na uelewa mpana wa wanachokiandika ili kuondokana na dhana ya upotoshaji.

# Aagiza halmashauri kuwafunda madiwani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU MKUU wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Mhandisi Joseph Nyamhanga, ameziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafuta fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo elekezi kwa madiwani wote nchini ili kuwepo na ufanisi kwenye Halmashauri zao.

Mhandisi Nyamhanga aliyasema hayo jana kwenye Mahafali ya 12 ya Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, jijini hapa.

Alisema ili kuwapo na ufanisi wa usimamizi wa mamlaka hizo, chuo hicho kina wajibu wa kutoa mafunzo licha ya kwamba kuna mafunzo ambayo yameandaliwa kutolewa kwa kutumia mfumo wa ujifunzaji wa kielektroniki (MUKI) lakini yanategemea upatikanaji wa mtandao.

Katibu Mkuu huyo alisema ni vyema mamlaka hizo zikafanikisha upatikanaji wa fedha ili kutoa mafunzo hayo elekezi.

Pamoja na hayo, Mhandisi Nyamhanga alizitaka halmashauri kuangalia namna ya kuwapa kipaumbele wanafunzi wanaohitimu fani mbalimbali kupitia chuo hicho kwenye nafasi za ajira kwa kuwa ni wabobezi kwenye taaluma ya serikali za mitaa.

Alipongeza uongozi wa chuo hicho kwa kupata mafanikio ikiwamo upanuzi wa chuo , kuongeza udahili, ufaulu wa wanafunzi, kuongeza watumishi na mpango wa kuongeza wigo na ubora wa mafunzo.

Hata hivyo, alisema mafunzo ya shahada ya kwanza yatakidhi mahitaji ya sasa ya kuboresha utoaji wa huduma na kutatua kero mbalimbali zinazokabili Mamlaka hizo.

Awali, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Mpamila Madale, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 chuo kilidahili wanafunzi 7,666 ikiwa ni ongezeko kubwa kulinganisha na mwaka 2007/8 chuo kilipoanza kutoa mafunzo kikiwa na wanafunzi 86.

## Asema uvuvi Zanzibar utakuja ajira, uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Abdallah Hussein Kombo, amesema endapo Zanzibar itajikita zaidi kwenye za uvuvi, kutakuwa na ukuzaji wa ajira na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Waziri huyo jana alianza kutekeleza maagizo aliyoyatoa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kuhusu kukutana na wadau wa uvuvi wakiwemo kampuni ya uvuvi ya Salmini, wavuvi na benki ya Equity.

Akizungumza katika uzinduzi wa uvuvi na mikopo kwa wavuvi uliondaliwa na benki hiyo ya Equity, Waziri huyo alisema serikali imeamua kujikita kwenye uchumi wa bluu na tayari imeonyesha ishara nzuri mpaka sasa.

"Kampuni ya uvuvi ya Salmini imepata soko la samaki aina ya jodari Finland, Uturuki na China na kwamba kila mwezi zinatakiwa tani 5,000 hivyo kampuni hiyo imepanga kununua samaki kwa wavuvi wadogo," alisema.

Waziri huyo alisema licha ya kuwapo kwa fursa hiyo, pia benki ya Equity imeonyesha utayari wake wa kutoa mikopo kwa wavuvi kwa ajili ya zana za kisasa za uvuvi.

"Mimi ninaomba kampuni za uvuvi ikiwemo Salmini, wavuvi na benki ya Equity kushirikiana kupitia kamati za wavuvi zilizoko vijijini ili kutimiza azma ya serikali kupitia uchumi wa buluu," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya nane imeamua kujikita kwenye uchumi wa buluu kupitia sekta ya uvuvi ili kukuza ajira na uchumi wa Zanzibar.

"Zanzibar ina zaidi ya wavuvi 50,000 hivyo kuna haja wadau wa sekta ya uvuvi kukutana na kamati za uvuvi ili kuona namna ya kunufaika na uchumi wa buluu ambao unajumlisha pia suala la ufugaji wa samaki na si uvuvi tu pekee yake," alisema.

Waziri huyo alisema kuna haja ya kuona wadau hao wanakutana mara kwa mara ili kuharakisha suala la upatikanaji wa fedha katika miradi mbalimbali ya sekta ya uvuvi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Equity, Robert Kiboti, alisema wamejipanga katika kuwawezesha wavuvi wadogo kunufaika kupitia uchumi wa buluu.

Alisema benki hiyo iko tayari kuunga mkono kipaumbele cha serikali ya Zanzibar ya uchumi wa bluu kwa kuwapatia mikopo wavuvi ikiwamo ya zana za kisasa za uvuvi.

# Akemea kufanya kazi kwa mazoea

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKUU wa taasisi za umma wametakiwa kutekeleza dhima ya kuwasimamia watendaji wao ikiwamo miradi ya maendeleo na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kwenda sambamba na kasi ya serikali.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha salamu za shukrani za Rais wa Zanzibar za kuwapongeza viongozi na wananchi Kisiwani Pemba kwa kukamilisha uchaguzi mkuu katika misingi ya amani alipokuwa akizungumza na wakuu wa taasisi za serikali.

Alisema nidhamu ya kazi lazima irejee sehemu za kazi kwa kuzingatia utaratibu unaompa fursa kila mtumishi kuangalia upungufu unaomzunguuka katika eneo lake la kazi na kuchukua hatua za uamuzi katika kutafuta suluhisho.

Hemed alisema watendaji lazima wabadilike vinginevyo utaratibu wa serikali utawabadilisha ingawa dharura za kibinadamu zinakubalika, alisema hakutakuwa na kisingizio cha mtumishi kuepuka wajibu aliopangiwa.

Makamu wa Pili huyo alisisitiza umuhimu wa kudumisha umoja na ushirikiano ambao ndio nguzo ya kufanikisha changamoto zinazojitokeza ndani ya jamii na hata taasisi za umma.

Alisema kuna uwezekano mkubwa wa changamoto zinazowakabili watendaji wa taasisi za umma na wananchi akatolea mfano wa huduma za maji, afya na miundombinu midogo inayoweza kutatuliwa kwa nguvu za viongozi katika ngazi za wilaya na mikoa.

Hemed alisema changamoto kubwa za wananchi zinapaswa kuwasilishwa katika ngazi za juu za serikali kwa hatua ya kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othman, kwa niaba ya wakuu wa taasisi zote kisiwani humo, aliwapongeza Rais John Magufuli na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kwa ushindi mkubwa walioupata kwenye uchaguzi mkuu uliomalizika hivi karibuni.

Alisema ushindi huo umedhihirisha wananchi wengi bara na Visiwani walivyo na kiu ya kuendelea kuwa na imani na matumaini na Chama Cha Mapinduzi kuendelea kuongoza dola nchini Tanzania.

Omar alisema wako tayari wakati wowote kupokea maagizo, mawazo na maelekezo ya viongozi wao katika kuchapa kazi kuanzia sasa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (katikati), akizungumza na watendaji mbalimbali wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, katika Ofisi ya Jaji Mkuu wa Zanzibar Vuga jana. Kushoto ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataka ushirikiano na uzalendo

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora, Haroun Ali Suleiman, amewataka viongozi na watendaji wa wizara hiyo kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na uzalendo ili kutekeleza vyema majukumu yao.

Waziri Haroun aliyasema hayo jana ofisini kwake Mazizini katika hafla ya makabidhiano kati yake na aliyekuwa waziri wa wizara hiyo, Issa Haji Gavu, yaliyohusisha pia taasisi za Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO).

Alisema maagizo yaliyotolewa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa mawaziri wakati wa kuapishwa yana lengo la kuwataka watendaji wote wa serikali kutekeleza vyema majukumu ili kuleta tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Haroun aliwataka kila mmoja kuwajibika kwa nafasi yake, huku akionya kutofadhaika katika utekelezaji wa majukumu yao kutokana na mchakato wa uteuzi wa watendaji wa serikali unaoendelea.

Alisema ni jambo la faraja kwa hatua ya Rais Mwinyi kuzipeleka taasisi hizo katika wizara hiyo .

Naye Gavu aliwashukuru viongozi na watendaji wote wa iliyokuwa wizara hiyo kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na upendo na kutaka kuhamishia juhudi hizo katika wizara hiyo mpya.

Alisema ana imani kubwa kuwa yale yote mazuri waliyomfanyia na kufanikisha utekelezaji mzuri wa majukumu yake, watayaendeleza chini ya uongozi wa Waziri Haroun.

Pia alimtakia Haroun utekelezaji mwema wa majukumu yake na kubainisha imani aliyo nayo katika kuendeleza na kukamilisha mchakato wa sheria ya GSO aliyoiasisi.

Katika hafla hiyo, Gavu alimkabidhi Waziri Haroun nyaraka mbili kutoka taasisi za Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO) ambamo ndani yake kumebainishwa bajeti, changamoto na mafanikio ya ofisi hizo.

Wakati huo huo, Gavu alikabidhi taasisi mbalimbali kutoka iliyokuwa wizara hiyo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uchumi, Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga.

Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Faragha, Habari na Mawasiliano Ikulu, Idara ya Mipango; Sera na Utafiti , Diaspora na Ofisi Kuu Pemba.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Soraga aliahidi kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na watendaji wote wa wizara hiyo, huku akisisitiza umuhimu wa wafanyakazi hao kufanyakazi kwa pamoja.

Alisema suala la mawasiliano ili kufikia uamuzi sahihi kiutendaji ni muhimu katika mustakbali mwema wa nchi.





Nipashe
BT
UDANI TELE

JUMAMOSI NOVEMBA 28, 2020



**LEBO KUBWA**

# Zinapowawinda Ma-RC wa Dar

MTU akiteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, tambua ana majukumu mazito kiasi cha kufananisha na nafasi ya uwaziri.

Kutokana na hadhi ya nafasi hiyo, tasnia ya sanaa ya muziki imejikuta ikiwatumia viongozi hao kwa namna mbalimbali ili kuiinua na kuiendeleza.

Hata lebo kubwa za muziki za Wasafi na Konde Gang, zinaendelea na ushindani wao kwa kuwakamata viongozi hao kuwaingiza katika himaya zao.

Mfano lebo ya WCB ilimshika vilivyo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ambaye ilimtangaza kama mlezi wao.

Baada ya kuondoka, kisha nafasi yake kujazwa na Abubakar Kunenge, 'Konde Gang', haikuzubaa kwani mara moja ilimfanya kuwa mlezi.

Lengo la kumkimbilia Mkuu wa Mkoa, halafu kumpatia kofia ya ulezi ni katika hatua ya kujitanua kwa kupata ushauri, kazi na ulinzi.

Kuteuliwa kwa Kunenge kuwa mlezi wa Konde Gang, ni wazi atakuwa mwepesi kuwapa ushauri pale anapoona wanakwenda vibaya pamoja na kuwaunga mkono katika kazi mbalimbali.

Kwa maana halisi, Harmonize, atakuwa amelamba dume muda mfupi tu tangu aanzisha lebo hiyo ndani ya mwaka huu.

Konde Gang ina wasanii sita ambao ni Harmonize, Ibraah Tz, Young Skales, Country Boy, Cheed na Killy.

BASI SAWA

## 20 Cent miaka ilee wangekuelewa

MKONGWE wa muziki wa BongoFleva, ameamua kujibu maswali ya watu waliokuwa wakijiuliza gari jipya analolimiliki limetokana na kazi gani anayofanya.

Akizungumza na EATV, msanii huyo ambaye alipata umaarufu miaka ya nyuma, amesema gari hilo aina ya Harrier, amepewa na ndugu yake limsaidie kwa usafiri.

"Mimi natumia tu hilo gari, sijui hata gharama zake, nipo nayo wiki ya pili sasa natembelea nayo, kuna wengine wanazo kama 10 au 15 ndani kwao wanakupa tu utembelee nayo, mimi sio kiben-ten ni mchapakazi lakini natokea kwenye familia zenye uafadhali kuna wakati siimbi lakini kwetu sikosi pesa ya mafuta," amesema



## Magumu anayopitia S2Kizzy

PRODYUZA maarufu S2Kizzy, amesimulia magumu anayopitia baada ya stuio yake kuvamiwa na kuharibiwa vifaa.

Amesema katika kipindi chote amekuwa na kazi ya kutafuta kazi za watu ambazo zimepotea pamoja na kununua vifaa kwa ajili ya kuanza kazi yake rasmi.



"Nimejifunza kuwa watu wajipange, maproducer wawe na vifaa vya kutunzia kazi, ulinzi pia ni muhimu katika kila ofisi kwani nyimbo nyingi zimepotea tunajitahidi kutumia njia moja au nyingine vitu vyote vikae kwenye mstari". Amesema S2Kizzy.



## Mkali Wenu hata Kiba unamfanyia usanii?

MCHEKESHAJI Mkali Wenu, amemfanyia usanii mwanamuziki Ali KIba, baada ya kudai wimbo wake mpya 'Mediocre' ameuandika yeye na ilikuwa chupuchupu kumpa Nay wa Mitego.

Amesema yeye na Kiba ni marafiki na kumpatia wimbo huo si kwamba yeye hana sauti ya kuimba, ila inatokana na ukaribu alionao ambao umekuwa kama ndugu.

"Kumuandikia mtu haimaanishi kama hauna sauti ila Alikiba yeye ana sauti nzuri, mimi nina sauti ila sio nzuri kwenye kuimba, nyimbo ya mediocre imekaa vizuri kwake nilishawahi kumpa Nay wa Mitego akasema haiwezi kuiimba".

## Adui ndani ya... Mabaya, mema hulipwa hapa duniani

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote mabaya yote ambayo utamfanyia binadamu mwenzako, kabla hata kulipwa mbinguni, utaanza kulipwa hapa hapa ulimwenguni.

Jamii mbalimbali duniani, imethibitisha hilo, kwani watu wengi ambao wamewahi kuwafanyia wenzao mbaya duniani, yamewakuta makubwa hapa hapa na wakabaki wanaadhirika.

Umeshawahi kuitazama filamu ya 'Adui Ndani Ya...?' Mtunzi alitaka ujumbe wake uwaendee walimwengu, ili wajue jinsi gani ya kuishi na watu duniani.

Dunia ni uwanja wa kupita tu. Haifai watu kutendeana ubaya. Ni filamu iliyochezwa na baadhi ya wasanii maarufu mama Hashim Kambi, Nisha, Flora Mvugi, Fadhili Maogola, Rashid Jabu, Makiragi Makiragi, Mzee Ulaiti, Justice Musiba, Latifa Issa, Robert Mlambala na wengine.

Inaanza kwa kumuonyesha msichana mdogo wa darasa la tatu hivi akiingia ndani kwao kutoka shule. Lakini anakuta baba yake amenyong'wa sebuleni. Anaingia chumbani anakuta mama yake na dada yake wamewekwa chini ya ulinzi na mzee Kambi, pamoja na mkewe. Kama vile haitoshi, msichana akiwa na sare zake za shule anashuhudia mama yake pia anauawa kwa bastola. Kilichotokea ni kwamba na yeye anachukuliwa mzobemzobe pamoja na miili ya wazazi wake na kwenda kutupwa porini. Walijua na yeye pia anaweza kuliwa na wanyama wakali. Haikuwa hivyo. Msichana huyo Linda, anaokotwa na wanakijiji cha jirani. Mzee Ulaiti anajitolea kumtunza, licha ya kupata upinzani mkali kutoka kwa mkewe na mabinti zake wawili. Mkewe inafikia wakati anahisi kuwa huenda ni mtoto wa nyumba ndogo kwa jinsi alivyompenda.

Miaka 10 baadaye, mzee kambi anampokea kijana wake Tonny aliyetoka Ulaya kwa masomo. Siku chache baadaye anapata ajali ya gari. Gari lake inaungua. Mzee Kambi na mkewe wanadhani amefariki. Lakini kumbe Tonny alijikokota porini na kwenda kuishia kwenye kijiji alicho Linda.

Anapokewa na mzee Ulaiti ambaye anampa chaguo la kuchagua msichana na kurejea naye mjini, pale atakapopona kabisa. Anamchagua Linda kati ya mabinti watatu. Hata hivyo Linda wakati huo ameshakuwa kiziwi na bubu kutokana na kadhia aliyoipitia, akishuhudia wazazi wake wakiuawa.

Hata hivyo haikuwa shida kwa Tonny. Alipopona akamchukua hadi mjini. Linda akakumbuka kila kitu, kuwa ameletwa kwenye familia ambayo iliwaua wazazi wake.

Ikawa shehere kubwa, mzee Kambi kumuona tena kijana wake aliyedhani kuwa amekufa kwa ajali.

Dunia haina siri na siri si ya watu wawili. Mzee Kambi na mkewe anakuja kugundua kuwa msichana aliyeletwa na kijana wao ndiyo yule ambaye zaidi ya miaka 10 iliyopita waliwaua wazazi wake.

Juhudi za kutaka kumuua zilishindikana kutokana na Tonny na dada yake Liveness kusimama imara kumlinda Linda. Wauaji wa kukodishwa wanashindwa na Mzee Kambi na mkewe anauawa.

Kisa ni kwamba mzee Kambi na mkewe wanaua watu kutokana na kumuabudu shetani.

Tonny anampenda Linda, anampeleka hospitali na anapata kusikia na kuongea.

Linda anamkumbuka mzee Ulaiti, anarejea kijijini kumtazama mzee wake, lakini pia kumwonyesha mchumba wake mpya, ambao wote ni wale waliowapokea na kuwasaidia walipokuwa na shida.





## Video 'Jini Babah' kukamilika Desemba

MWANAMUZIKI anayekuja juu kwa kasi, Joshen Adam, maarufu kama Giny, amesema hivi karibuni video ya wimbo wake 'Jini Babah' itakamilika.

Akizungumza na BT, Giny, amesema kila kitu kuhusu video hiyo inakwenda vizuri na kuanzia mwezi unaokuja itakuwa tayari.

"Nipo katika harakati kubwa ya kukamilisha video ya wimbo wangu, uongozi wangu unasimamia vizuri kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri na nina imani mwezi unaokuja tutaitambulisha rasmi," amesema Giny.

## WALIOFANYA KAMA KOFFI NA DIAMOND

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI maarufu Afrika na duniani kwa ujumla, Koffi Olomide, wiki iliyopita alikuwa yupo nchini Tanzania kwa ajili ya kutoa wimbo wa pamoja 'collabo' na msanii maarufu nchini na Afrika, Diamond Platinumz.

Ngoma hiyo ambayo imeanza kusumbua inaitwa 'Waah.'

Ukiusikiliza wimbo huo, yoyote atakayesema kuwa ni 'remix' ya 'Papa Mobimba', hatakuwa amekosea.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa Koffi pia ana ngoma nyingine ambayo ameshirikiana na msanii wa kike 'Nandy', nayo ipo kwenye hatua ya kuchukuliwa picha za video.

Ujio ya Koffi ambaye ni mwanamuziki kutoka Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Kongo kufanya muziki na wasanii wa Watanzania si wa kwanza kwenye historia ya muziki nchini Tanzania.

Wanamuziki kadhaa kutoka Kongo wameshawahi kuja nchini na kufanya muziki na wanamuziki wa Tanzania, wengine walirekodi na wengine hawakubahatika. Tofauti ni kwamba walifanya muziki na wanamuziki wa dansi, badala ya bongo fleva ambayo wakati huo haukuwapo.

**Sam Mwangwana na Maquiz du Zaire**

Mwanamuziki maarufu nchini Kongo, Sam Mangwana, aliyepigia bendi zote kubwa nchini humo, TP Ok Jazz ya Franco, na Afrisa International ya Tabu Ley, alishawahi kuja nchini mwishoni mwa miaka ya 1980 na kujiunga na bendi ya Maquiz du Zaire. Alifanya kazi nayo sana na kusafiri karibuni mikoa yote na hata nje ya nchi. Kwa bahati mbaya hakurekodi nao.

**Sam Mangwana na Vijana Orchestra**

Mangwana huyo huyo ambaye aliishi sana nchini Tanzania maeneo ya Manzese na hata akapataja kwenye wimbo yake ya 'Kabibi' akisema 'Kamanga wangu Manzese', akimtaja Kamanga ambaye alikuwa mfadhili wake, alirejea nchini na kujiunga na bendi ya Vijana Jazz. Hili kuwa halisemwi sana, lakini mwanamuziki huyo ndiye aliyeibadilisha Vijana Jazz aina yake ya mapigo na uimbaji na alishiriki kutengeneza vibao kama 'Bujumbura', 'Mary Maria', 'Tambiko La Pambamoto', ambazo ziliibadilisha sana bendi hiyo na kuanza kuwa tishio nchini.

**Mayaula Mayoni na MK Beats**

Huyu anakumbukwa mwishoni wa miaka ya '60 alikuwa mchezaji wa Yanga. Baadaye baba yake aliyekuwa akifanya ubalozi wa Kongo alipoondoka aliondoka na kijana wake. Miaka ya '70 akaibuka kuwa mwanamuziki maarufu sana akihudumu kwa Franco Ndiyo mtunzi wa wimbo wa 'Mbongue' uliopata umaarufu sana miaka ya 1990. Alirejea nchini katikati ya miaka ya 1990 na kujiunga na MK Beats. Sikiliza wimbo wa 'Tucheze Sote Tukunyema' akitajwa. Alifariki mwaka 2010 nchini Ubelgiji.

**Bozi Boziana na Twanga Pepeta**

Ni mmoja wa wanamuziki waliopata umaarufu sana nchini kwa wimbo wake ya 'Tembe na Tembe' uliopendwa sana.

Mkongomani huyu alifanya ziara nchini na kutengeneza wimbo aliouita 'Dar es Salaam' ambao aliimba kiswahili akimtaja Asha Baraka ambaye alimleta. Pia aliwahi kutoa albamu na African Stars 'Twanga Pepeta' mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**Madilu System na Borabora Sound**

Mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2000, mwanamuziki mwingine Mkongomani, Madilu System alikuja mchini na kutoa wimbo mmoja uliosumbua wakati huo ukiitwa 'Eloa', akiupiga akiwa na bendi ya Tanzania, Borabora Sound.



## Linda wewe mrembo wa Afrika



MWIGIZAJI mkali kutoka Nollywood, Linda Osifo, amesema akiwa shuleni alidhalilishwa kutokana na kuwa na alama alizopewa kama mila ya kabila lake.

Akitumia ukurasa wake wa Istagram, mrembo huyo wa filamu za Kinigeria, amesema utani aliopewa na wanafunzi wenzake ulimnyima raha hadi akafikiria kufanyiwa upasuaji ili kuziondoa.

"Alama za kikabila zilinipa shida kwangu, wakati nikiwa shule ya msingi huko Canada, nakumbuka nilichekwa kutokana na alama zangu za kikabila na kuulizwa ikiwa nilivamiwa na simba huko Afrika. Utani ulizidi kuwa mbaya hata nikajaribu kuziondoa," amesema.



## 9ice usirudie kuchepuka

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria, Alexander Adegbola Akande maarufu kama 9ice, amejitokeza na kumuomba radhi mkewe, Sunkami.

Katika video ya karibu dakika mbili, msanii huyo alimtaka mkewe amsamehe kwa jambo baya alilofanya la kujihusisha kimapenzi na mwanamke mwingine.

"Nimefanya kitu cha aibu sana, cha kutisha sana, na ikinigharimu mimi na familia yangu. Jambo muhimu zaidi ni familia yangu hasa wewe mke wangu," amesema.

## Meghani asimulia alivyoanguka sakafuni

MWIGIZAJI na mke wa mwanamfalme wa Uingereza, Meghan Markle, ametoboa siri kwamba hivi karibuni alianguka na kutishia uhai wa mtoto wake wa pili.

Meghan amesema miezi michache iliyopitia alikuwa katika wakati mgumu kufuatia tukio hilo, lakini mume wake Prince Harry, alikuwa karibu naye akimfariji.

Kwa mujibu wa Meghan, alikuwa akimtayarisha mtoto wake wa kwanza Archie katika nyumba yao iliyopo Los Angeles, lakini kwa bahati mbaya aliteleza na kuanguka chini.

"Nilihisi tumbo limeshuka sakafuni nikiwa na mtoto mikononi mwangu, nilipiga kelele ili kuwatuliza wote wawili," amesema Meghan.





## Duncan kwa nini unawadunda wenzio?

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Duncan Mighty, yupo matatani baada ya kutuhumiwa kumshambulia naodha wa meli huko Port Harcourt.

Katika chapisho kupitia Facebook, Ndubueze Obodow amedai mwanamuziki huyo kumshambulia nahodha hiyo, Okabam John.

"Kulingana na dereva wa gari moja la maji safi, alikuwa Duncan ambaye alimpiga kichwa naohodha huyo huu akilindwa na walinzi wake," alisema.

## Charles umefanya uungwana

MSANII mkongwe wa muziki kutoka Nigeria, Charles Oputa, ameamua kuchukua jukumu la kuomba radhi baada ya binti yake kuchafua hali ya hewa kwa kuanika picha zake za ngono.

Katika posti yake kwenye ukurasa wa istagram, mwanamuziki huyo alimuombea radhi mtoto wake huyo kwa kufanya tukio hilo la kufedhehesha.

"Mpendwa Dewy, najua siku chache zilizopita ulikuwa na wakati mgumu , kwa wazazi namuombea radhi kama posti yake ilikuwa mbaya , naomba samahani sana , nisameheni," ameandika.



MAKALA



Mji Mikelle ukiwa tupu baada ya raia kukimbilia nchi jirani ya Sudan.

# KINACHOJIRI TIGRAY

## ■Amri kushambuliwa mji kuu yatolewa rasmi
## ■Hofu yatanda kote, raia wajikusanya kujilinda

WIKI hii Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, ametangaza kuanza kwa awamu ya mwisho katika operesheni ya kijeshi ya kuung'oa utawala wa chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), kinachoongoza jimbo la Tigray.

Katika kukamilisha mpango huo, mji mkuu wa jimbo hilo Mekelle unalengwa na vikosi vya jeshi la `serikali ya Shirikisho, ili kukamilisha uasi wa chama hicho kikongwe nchini humo. Katika tangazo lake, Abiy Ahmed, amesema wanajeshi watajaribu kushambulia mji huo kwa tahadhari ili wasiwajeruhi raia na ametoa wito kwa watu kubaki ndani ya nyumba zao.

Hatua hilo inajiri baada ya muda wa mwisho uliyotolewa kwa wapiganaji wa Tigray kujisalimisha kumalizika siku ya Jumatano. Hata hivyo, chama cha TPLF, ambacho kinadhibiti mji wa Mekelle, kimeapa kuendelea na mapigano.

Taarifa kutoka ndani ya jimbo hilo ambalo limeachwa bila ya mawasiliano ya Intaneti kwa muda mrefu, inasema mamia ya watu wameripotiwa kuuawa na wengine maelfu kukimbilia nchi jirani ya Sudan. Kabla ya kutangaza kuushambulia mji huo wenye wakazi zaidi ya 500,000, wanajeshi wa muungano vya Ethiopia wameteka miji kadhaa ya jimbo hilo ambayo ilikuwa mikononi mwa wapiganaji wa TPLF.

**ITAKUWA RAHISI KUUTEKA?**

Kwa mujibu wa wachambuzi wa masuala ya migogoro, wanasema itakuwa vigumu kwa wanajeshi wa serikali kuuteka mji wa Mekelle kwa urahisi kutokana na wapiganaji wa chama hicho kujizatiti ndani ya mji huyo.

Wanasema tofauti na dhana inayotolewa, mapigano katika kuumiliki mji huo utahitaji mbinu za ziada kutokana na jiografia yake kuwa ngumu na yenye kutia hofu.

"Mekelle ni mji unaozungukwa na milima mingi, wanajeshi wa serikali wanahitaji kuwa na mbinu ya hali ya juu kuingia na kuwadhibiti wapiganaji wa TPLF, ambao ni wazuri kwa vita ya milimani," anasema Federick Kauzula.


Anasema kutokana na ugumu wa mawasiliano ndani ya jimbo hilo, itakuwa vigumu kuthibitisha kuwa vikosi vya serikali viko karibu au vinajiandaa na mapigano ya mbali kwa kutumia vifaru, ndege vita na makombora.

"Kwa kutumia mbinu ya kushambulia kwa mbali, athari kwa raia itakuwa kubwa hasa kwa kuzingatia watu wengi watakuwa wameshindwa kuondoka na kubaki ndani ya nyumba zao," anaendelea kusema.

**WATIGRAY WAJILINDA**

Wakati tangazo hilo likitolewa, viongozi wa Tigray wamewaagiza wananchi kujikusanya na kujilinda dhidi ya vikosi vya serikali kuu. Kwa ujumla, hofu ya vita imetanda ndani ya mji huo na kuwafanya wananchi kujiandaa kwa kuchimba mahandaki kwa ajili ya kujilinda.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Abiy



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed.

Ahmed, amekataa maombi yanayotolewa na mataifa mbalimbali kufanyika kwa mazungumzo ya kumaliza mgogoro huo.

Anasema hakuna nchi itakayoweza kuwapangia kitu gani cha kufanya wakati wanataka kuilinda nchi yao dhidi ya mgawanyiko wa kikabila.

TPLF ilitangaza hali ya hatari tangu mwanzo ikidai inatetea usalama wa watu wake. Serikali kuu inasisitiza kuwa vita vyao ni dhidi ya serikali ya eneo hilo na wala sio watu wa Tigray.

**UMOJA WA MATAIFA YAONYA**

Umoja wa Mataifa imeonya kwamba huenda hali itakuwa mbaya kama mji huo utashambuliwa kutokana na msaada wa kibinadamu uliopo kwa sasa unafikia ukingoni. Katika taarifa yake inasema maelfu ya watu kaskazini mwa Ethiopia, wako katika hatari ya kufa kwa njaa kutokana na mapigano yanayoendelea.

"Kunasemekana kuna ukosefu wa bidhaa muhimu kama vile unga na mafuta," Mkurugenzi UN nchini humo, Catherine Sozi, ameiambia **BBC.**

**MGOGORO ULIANZAJE?**

Mwaka jana Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, mara alipoingia madarakani alivunja muungano uliounda serikali uliojumuisha vyama vilivyoundwa kwa misingi ya kikabila, kisha aliiunganisha katika chama kimoja kinachoitwa, National Party.

Hata hivyo, viongozi wa TPLF walikataa kujiunga.

Utawala wa Tigray unaona mageuzi yanayofanywa na Abiy ni kama jaribio la kujenga mfumo wa serikali moja na kuharibu wa sasa wa shirikisho.

Pia viongozi hao wamekasirishwa na urafiki wa Waziri Mkuu huyo na Rais wa Eritrea, Isaias Afwerki.

Kwa upande wake wa Abiy, anaamini kuwa maofisa wa TPLF wanahujumu mamlaka yake.

Amekasirishwa na matendo yao kiasi ambacho alimuru mashambulio ya kijeshi dhidi ya TPLF baada ya kusema kuwa wapiganaji wake walikuwa wamevuka kwa kushambulia kambi za jeshi.



Baadhi ya raia wa Tigray wakiwa wamepumzika baada ya kuukimbia mji wa Mikelle.



Baadhi ya wanajeshi wakiangalia namna ya kuanza mashabulizi.

# Masomo chekechea, mzizi unaoumba Mkoa Kagera kung'ara elimu ya taifa

## ■Wazawa waorodhesha vidokezo vinavyowabeba

**Na Jaliwason Jasson,** BUKOBA

KAGERA imo katika mkoa ambao nao 'si haba' kwa idadi kubwa ya wasomi nchini, ni ngumu kuiacha mkoa.

Hapo napo kuna lingine, elimu ya awali inatajwa kichocheo kikubwa kinachosaidia ufaulu wa mkoa, kupitia kipaumbele inachopewa kuwajengea msingi mzuri wanafunzi mkoani.




**WAZAZI & WALEZI**

John Rwehabura, mkazi wa Hamgembe mjini Bukoba, anasema elimu ya awali imekuwa ikiuvusha mkoa, kwani kuna michezo inayowavutia wanafunzi na kuwafanya wapende kuhudhuria masomo.

Rwehabura anataja kingine, ni kuwatumia walimu wa muda mrefu na waliobobea kufundisha wanafunzi wa ngazi hiyo ya chini, wengi kiumri watu wazima wenye mbinu nyingi zisozowachosha wanafunzi.

Anasema, wanafunzi wa awali wanapojengewa mazingira rafiki ya namna hiyo, wanaipenda shule na masomo yake, wakipaona mahali salama kwao, hali inayowarahisishia jukumu la kufunza, kuliko kuegemea adhabu

Mkazi wa Kibeta mjini humo, Jackline Rwezaura, anasema ili mwanafunzi wa awali afanye vizuri masomoni, ni lazima kwa wazazi na walezi wamjengee mazingira rafiki kuanzia nyumbani.

Hapo anayataja mahitaji, kama vile vifaa vya kucheza na masomoni, ili apate shauku ya kwenda shule kukutana na wenzake.

Mzazi huyo anasema kazi kuu ya kwanza ya mzazi ni kumjengea nidhamu mtoto akiwa nyumbani, ambayo baadaye inabeba matokeo chanya shuleni na inamsaidia akutanapo na wenzake.

Kwa vipi? Mzazi huyo anafafanua kuwa ni pamoja na kumuongeza mtoto huyo uelewa na ujuzi wa vitu kutoka kwa walimu, pia wanafunzi wenzake.

Ni wazo linalochukua sura pana kumfikia mkazi wa Bugabo, Mulokozi Mwemezi, anayechangia mada kuwa mbinu pekee iliyowavusha vijana wakafaulu vizuri masomo, ni pale serikali ilipotangaza elimu bure kuanzia msingi hadi kidato cha nne.

Mwemezi anasema imejenga hamasa kwa wazazi wanaochangamkia fursa hiyo, kuwapeleka watoto wao kuanza shule za chekechea zinazowapatia sifa kujiunga za darasa la kwanza.

Mkazi wa Izimbya, Renatha Joseph, anasema ni busara kumuanzisha mtoto chekechea, kwa kuwa anaandaliwa msingi bora wa kielimu kwa ngazi zinazofuata.

Hata hivyo, ana angalizo kuwapo kuna wazazi wanaowapeleka watoto wao katika elimu ya awali kwa lengo la kupunguza usumbufu wa malezi, wabaki huru kufanya kazi zao, lakini wanajikuta kufaidika na watoto kunasa msingi mzuri wa elimu.

Jonathan Kajala, anayeishi Kikukwe, manispaa ya Bukoba, anataja lengo la wazazi wengi kupeleka watoto shule hizo, pia ni fursa ya kuwakuza kimaadili, matunda ambayo sasa mkoa Kagera unayafaidi kwa ufanisi katika elimu ngazi za ngazi za juu.

Kajala anasema, historia ya mkoa ni kwamba una idadi kubwa ya wasomi, mzizi wake ni hamasa ya wazazi kuwapeleka watoto shule tangu umri mdogo

**WAKONGWE & WASTAAFU...**

Mwalimu Ernest Kato, kutoka wilayani Muleba, anayejitambulisha kafundisha darasa la awali kwa miaka 30, anataja hatua hiyo ndiyo msingi mkuu wa ngazi zote za elimu.

Anataja kinachoisaidia Kagera kufanya vizuri ni namna wanavyowatumia walimu wenye weledi na wanaojua stadi za maisha, ambao wamekuwa wakifundisha madarasa ya awali. Mwalimu Kato anataja kitu pekee kinachomfanya mwanafunzi wa awali aipende shule, ni upendo wa aina yake ili kila anapokutana na mwalimu, amuone rafiki wa karibu na daima siyo adui anyemuogopesha.

Anasema, matumizi ya zana za kufundisha nio njia pekee za kuwasaidia wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, pasipo mwanafunzi kutaabika anapofundishwa kinadharia.

Mwalimu Majid Mfinanga, anajitambulisha ni mkufunzi wa vyuo vya ualimu, anasema mwanafunzi wa chekechea hapaswi kuchapwa, hata kuona fimbo, kwani anapoiona inamjengeaa hofu kisaikolojia, itakayomfanya achukie shule.

Mfinanga anasisitiza matumizi ya zana za ufundishaji, mwanafunzi kupata uji masomoni, ni sehemu ya vichocheo vikubwa kwa mwanafunzi wa awali kung'ara katika kivuko cha kuingia darasa la kwanza, bila kuujua usumbufu wa mwalimu.



Wanafunzi wa chekechea mjini Bukoba wakiwa masomoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MKOA ULIKOSIMAMA?**

Takwimu za kitaifa za mwaka 2018, Kagera ilikuwa na ufaulu elimu ya awali imevuka malengo kwa asilimia 122.7, huku ufaulu wa ngazi hiyo kitaifa ni asilimia 100.

Kwa tathmini kuu, Mkoa wa Kagera ulikuwa umeshika nafasi ya tisa kitaifa na Ofisa Elimu Mkoa, Juma Mhina, anaiambia Nipashe kuna mbinu zilizofikisha mafanikio hayo.

Mosi, anataja uhusiano mzuri na jamii inayoishi karibu na shule za awali, inawasaidia kujua matatizo yanayowakabili wanafunzi wao na wanayatatua kwa wakati na kuleta chachu katika ngazi zote kijamii; kijijini, kitingoji, kata, tarafa, wilaya hadi mkoa kuibuka 'kidedea.'

Mtaalamu huyo wa elimu, anataja mbinu nyingine ni kila shule kuhakikisha ina madarasa ya awali na kutosha, pia walimu ndani ya mazingira rafiki, huishia wanafunzi kufanya vizuri. Mhina anataja zingine ni mahudhurio mazuri ya wanafunzi, matumizi ya zana za kufundishia hususani madarasa yanayoongea na kuzingatia mitaala, ni nyenzo vitu muhimu ambavyo vimewasaidia kuvuka.

Ofisa huyo wa elimu anazitaja mbinu zingine ni kutoa motisha kwa walimu wa awali, akitoa mfano fursa za kwenda kusimamia mitihani ya kitaifa na nyinginezo.

Mbinu nyingine anataja ni kuhimiza uwajibikaji na ufuatiliaji walimu, ikiendana na mafunzo kwao ya elimu ya awali wakishirikiana na wadau wa karibu. Hapo wanatajwa wadau kama mashirika yasiyo ya kiserikali na wasimamizi wakuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wanaotoa mafunzo ya kuwaongezea uwezo kufundisha kwa weledi wanafunzi wa awali.

Kiongozi huyo wa elimu mkoani anahimiza upatikanaji uji shuleni kwa ajili ya kuimarisha lishe na afya ya wanafunzi wa awali, kunawapa weledi kunasa wanachofundishwa, ikionanishwa na miundombinu rafiki katika shule zao.

Takwimu za mwaka 2018 ni kwamba Kagera, iliandikisha wanafunzi wa awali 85,553; wavulana 42,678 na wasichana mkoa ukivuka lengo sawa na asilimia 103.3.

**WALEZI CHEKECHEA**

Mkurugenzi wa Kituo cha Kulelea Watoto cha Marian Daycare, David Kato, kilichopo Mjini Bukoba akizungumza na Nipashe, anasema wanafundisha ubunifu wanafunzi wao, jambo linalochangia wao kufanya vizuri kwa darasa la awali.

Pia, anataja kuwapo miundombinu rafiki kwa masomo ngazi hiyo na walimu wenye uzoefu, huku akihusisha na asili ya mkoa huo kuwa na historia ya jamii kukua na elimu.Mratibu wa Shirika la Kikukwe Community Development Innitiatives (KCDI), Christine Nyangoma, anasema wamekuwa wakiwasisitiza wazazi kuwatengenezea 'midori' watoto wachezee na kuwa wabunifu.

Nyangoma anasema, shule za awali zinapokuwa na viwanja vya kuchezea na wanafunzi wakapewa muda wa kucheza na kubuni itawasaidia kuongeza uelewa na ndicho wanachokifanya hata Kagera kunang'ara kielimu.

## HABARI KIMATAIFA

## Ujumbe wa Afrika wakutana na Abiy

**ADIS ABABA,** Ethiopia

WAJUMBE kutoka Umoja wa Afrika (AU) walikutana jana na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, siku moja baada ya kuamuru jeshi kuanza awamu ya mwisho ya mashambulizi katika jimbo la Tigray.

Mataifa mbalimbali na mashirikia ya utetezi wa haki za binadamu yanahofia mashambuluzi hayo huenda yakasababisha maafa kwa raia.

Msemaji wa kikosi kazi cha serikali cha hali ya dharura kuhusu mzozo wa Tigray, Redwan Hussein, alisema wajumbe hao walitarajiwa kukutana na Abiy mchana wa jana.

Wakati huo huo, watu wanaendelea kuukimbia mji mkuu wa Tigray, Mekele wakihofia mashambulizi kutoka vikosi vya shirikisho.

Mapigano yameripotiwa kufanyika nje ya Mekele, mji wenye watu karibu nusu milioni ambao wameonywa na serikali ya Ethiopia kuwa hawatahurumiwa kama hawatojitenga na viongozi wa Tigray. **DW**

## Ofisa wa Iran kushtakiwa Ubelgiji

**BRUSSELS,** Unelgiji

MJUMBE mmoja wa kidiplomasia wa Iran, amefikishwa mahakamani jana nchini Ubelgiji, akishtakiwa kupanga shambulizi la bomu nchini Ufaransa.

Assadollah Assadi, alishtakiwa kupanga shambuzi hilo katika mkutano wa upinzani nje ya mji mkuu wa Paris.

Hata hivyo kesi hiyo imeibua mvutano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili.

Mwanadiplomasia huyo kama akipatikana na hatia, atakabiliwa na kifungo cha maisha jela.

Katika tukio hilo lililotokea Juni mwaka 2018, maofisa wa Ubelgiji walidai kuzia jaribio la kuingiza mabomu nchini Ufaransa kwa njia ya magendo kwa lengo la kuushambulia mkutano wa wapinzani wa Iran wanoishi uhamishoni.

Kesi dhidi ya Assadi, inakuja siku moja baada ya makubaliano ya kubadilishana wafungwa na Thailand, raia watatu wa Iran waliondolewa baada ya kufungwa kwa kuhusika na shambulizi la bomu nchini Thailand mwaka 2012. **DW**

# Rais Bashar Al Assad sasa kuchunguzwa kwa mauaji

**BERLIN,** Ujerumani

WAENDESHA mashtaka wa Ujerumani wanachunguza ushahidi wa matumizi ya kemikali katika vita vya Syria.

Endapo uchunguzi huo ukikamilika na kuonekana ushahidi wa matumizi ya kemikali, Rais wa nchi hiyo Bashar al-Assad, anaweza kushtakiwa kwa makosa ya uhalifu wa kivita.

Shirika la Utangazaji la Ujerumani (DW) na gazeti la Der Spiegel, yamefanikiwa kuwahoji mashahidi na kupata nyaraka muhimu ambazo zinachunguzwa.

**Siwezi kusema kwamba sisi wenyewe tumethibitisha hilo, lakini hakika tuna taarifa zinazoonesha kuhusika kwake katika mashambulizi ya sumu ya sarin.**

Agosti 21, mwaka 2013 makombora yaliyokuwa na sumu ya sarin yalishambulia mashariki mwa Ghouta na kuua idadi kubwa ya watu.

Muuguzi mmoja, Eman, aliiambia DW kwamba watu wengi waliuawa barabarani, magari yalisimama, watu walijazana ndani ya magari ambapo wengine walikufa wakati wakijaribu kukimbia.

Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa vinavyojitegemea, takriban watu 1,000 waliuawa katika shambulizi hilo, wakiwamo zaidi ya watoto 400.

Ushahidi huo unachunguzwa na waendesha mashtaka wa Ujerumani ili kuanza kufungua mashtaka.

Robert Heinsch, Mkurugenzi wa Jukwaa la Kalshoven-Gieskes, linaloshughulika na Sheria ya Binaadamu ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Leiden, alisema kwa kuwa uhalifu wa kivita mara nyingi hufanywa katika mfumo wa vikosi vya kijeshi, sheria za kimataifa zinatambua kuwa makamanda wanaotoa amri wanahusishwa na ukiukaji kama huo.

"Watu wanaotoa amri kwa wanajeshi wa kawaida au yeyote anayehusika kwa kufanya mashambulizi, anaweza kushtakiwa kwa sababu ya vitendo vyake vya kuamuru. Au hata kama mtu hakuamuru mwenyewe, lakini alikuwa anafahamu au alipaswa kujua kuhusu mashambulizi. Kwa sababu ya kazi zao kama makamanda wa jeshi, wanaweza kuwajibika," alifafanua Heinsch.

Aidha, Steve Kostas, ofisa wa ngazi ya juu wa sheria katika Taasisi ya Haki ya Jamii, alisema kuwa wana ushahidi Rais Al-Assad anahusika katika kufanya uamuzi.

"Siwezi kusema kwamba sisi wenyewe tumethibitisha hilo, lakini hakika tuna taarifa zinazoonesha kuhusika kwake katika mashambulizi ya sumu ya sarin," alisema Kostas.

Kostas alibainisha kuwa wameonyesha kulikuwa na kitengo maalum kinachoitwa Tawi 450 ambacho kilihusika kupanga na kutekeleza mashambulizi ya silaha ya sumu ya sarin.

Alisema wameonyesha orodha ya makamanda waliohusika katika kitengo hicho na uhusiano wake na Ikulu ya Rais. **DW**



Raia wa Argentina wakigombea kulishika gari lilobeba mwili wa mwanasoka maarufu Diego Armando Maradona, wakati likiingia katika makazi ya Rais ya Casa Rosada, eneo la Buenos Aires juzi. Maradona alifariki kwa matatizo ya moyo akiwa na miaka 60. **PICHA: AFP**



# Trump atoa sharti kuondoka madarakani

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump (pichani), amesema ataondoka Ikulu kama rais mteule Joe Biden, atathibitishwa rasmi kuwa mshindi wa uchaguzi.

Hata hivyo, alirudia kusisitiza kwamba hawezi kukiri kushindwa uchaguzi huo.

Alipoulizwa na waandishi wa habari kama ataondoka Ikulu ya White House, iwapo kamati ya wajumbe maalumu maarufu Electoral College itathibitisha ushindi wa Biden, Trump alisema ataondoka endapo wajumbe hao watamthibitisha.

Alisema wakifanya hivyo watakuwa wamefanya kosa na yeye itakuwa vigumu kukubali.

Alirudia madai yake ya kuwapo kwa udanganyifu kwenye uchaguzi huo, bila kutoa uthibitisho.

Wakati wa kuadhimisha sherehe za Kutoa Shukrani inayofahamika kama Thanks Giving, Trump alifikia hatua ya kuifananisha miundombinu ya uchaguzi wa Marekani sawa na ile ya ulimwengu wa tatu. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**HIDAYA FARAJA MFINANGE** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0225/0030/2017** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **CAGLIERO GIRLS** mwaka **2017,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**DAR/URA/RB/824776/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



116017502

**MABANHA DOTTO GEREMA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.0609/0513** iliyotolewa na MATAI SEKONDARI mwaka 2020 pamoja na Leaving Certificate. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **URP/RB/6449/2020.**

## PASSPORT IMEPOTEA



116017602

**JUNIOR JULIANUS KIMODOI** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 039276** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam Julai 23, 2018. Muda wake wa kuisha matumizi ni Julai 22, 2028. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/823766/2020.**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**Katika Mahakama ya WILAYA – TEMEKE**
**MIRATHI Na. 116.... 2020**
**Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya Marehemu FURAHA ELIAS MAIGE**
**na**
**VAILETH ANDERSON KINYANGE.............. WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

**(Kanuni ya 75)**
Watu wote wanaodai kuwa na haki ya mirathi ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi 12, 2020.
Imewasilishwa leo tarehe 27 mwezi 11, 2020.

**THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**SONGEA DISTRICT REGISTRAR**
**AT SONGEA**
**RULE 13, Subordinate Court (Civil Produre)**
**DC PC CIVIL APPEAL NO 8/2020**
**ANGELINA CHOWO....................APPELANT**
**VERSUS**
**BLANDINA MGIMBA..................RESPONDENT**
**TO: BLANDINA MGIMBA**
**NOTICE OF DATE MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention on 23rd day of February, 2021 at 09:00 a.m Before Hon I. Arufani Judge.
You are required to appear in this Court without fail any and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my hand and the seal of Court this 24th day of November, 2020.

116018602

## VYETI VIMEPOTEA



**AYUBU GARBINDI** anatangaza kupotelewa na vyeti,cheti cha **KIDATO CHA NNE** chenye no S4706-0004 kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia **FAMGI SEKONDARI** mwaka **2014** na cha **KIDATO CHA SITA** chenye **No S0766-0548** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **KIMAMBA SEKONDARI** mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**DOD/DOD/RB/822361/202020.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



116018302

**FATMA MUSSA OMAR** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S 5114/0504** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary SUZA mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/823275/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCIS SALES MUTUNGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 364 BHP LANDCRUISER.** Chassis namba **JTECBO9JX012055.** Engine namba **1HZ0421887.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MAG/RB/825769/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVARIST JOHN NDALECHI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 354 AMT TOYOTA MARK II.** Chassis namba **SX813364503.** Engine namba **IG5874293.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI: DAR/MAG/RB/824788/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ERNEST SIMON GHULILA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 330 DHV** aina ya **TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/825366/2020.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SHARIFA ABDALLAH MPAYA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1282/0546** iliyotolewa na **UBIRI SEKONDARI** mwaka **2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**DAR/GOG/RB/823597/2020.**

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**ARIZINA MUSSA** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo. Cha kidato cha nne chenye index namba **P0222/0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya Sekondari Zanaki. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1072-0013** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Kamene. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/TAB/RB/226397/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

116017202

**WILSON SAMWELI RUHINDA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA WISH** yenye namba za usajili **T 272 CKQ** chasisi namba **ZNE100008404,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/823699/2020**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.64 OF 2020**
**In the matter of the Estate of the late SAIMON MHALU LUGANO of Kawaka Ward, Chamwino District within Dodoma Region.**
**AND**
**In the matter of an Application for letters of Administration by SARAH SAIMON LUGANO.**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before 16 Day of December 2020.
Dated at Dodoma this 16TH day of November 2020

116018102

**RE;THE LAND ACT NO 4 OF 1999**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF REF NO;MMC/LD/11346**
**REGISTERED OWNER; ROSEMARY JOSEPH**
**LAND; PLOT NO. 170 BLOCK 'A' KILIMANJARO MOROGORO MUNICIPALITY**
**APLICANT; ROSEMARY JOSEPH KIPETA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days(30) from the date of this pubication.
**THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found,should be delivered to the office of the ;Municipal Director,Morogoro Municipal Council,P.o box 166 Morogoro.

Mayugwa T.D
**For:- MUNICIPAL DIRECTOR**
**MOROGORO**

116018202

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-40

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

Na Adam Fungamwango




KUMUUA msichana kama yule ilionekana ni jambo dogo tu, japo ugumu ulikuwepo kwa sababu hakuwa peke yake. Lakini haikudhaniwa kuwa ingekuwa ngumu kiasi hicho.

Kutambaa kwa tumbo, kulimfikisha karibu na barabara. Karibu na eneo lile ambalo gari lake limeteketezwa na risasi.

Ni mita chache tu kutoka kwa watu sita, wanne kutoka kwenye gari na wawili kutoka kwenye bodaboda wakihangaika kutafuta waliokuwa wakiwatafuta.

"Kuweni na tahadhari. Na sasa natoa amri, wote wawili wakionekana wauawe." Eddy aliisikia amri hiyo.

Mmoja wa watu waliokuwa na bunduki aliruka mfereji wa maji uliokuwa kando ya barabara hiyo na kuelekea kwenye mti mmoja uliokuwa kando. Akiwa na tahadhari, lakini akijiamini kupita kiasi aliufuata mti huo kwa makini.

Eddy hakuna na bunduki. Alitaka kwa udi na uvumba. Kwa akili yake kikomandoo. Alichukua kijiwe na kukirusha upande wa kushoto huku yeye akiwa kulia.

Kishindo hafifu cha kijiwe hicho kilishtua jamaa mwenye bunduki. Akaangalia kushoto na kulia. Kwa akili yake alivyofundishwa ni kwamba jiwe likitupwa kushoto, basi mtupaji atakuwa yupo kulia.

Sivyo alivyofikiri. Eddy alishahama siku nyingi. Alivyorusha na yeye akaelekea upande huo huo kwa kutambaa.

Jamaa alipogeuka na kuelekea alipodhani ndipo kijiwe kilipotupwa, Eddy alimfuata taratibu akiwa anatambaa kama mamba anavyowinda.

Ghafla alisimama. Wakati jamaa akihisi kama kuna kitu nyuma, tayari alikuwa amepigwa karate ya kichwa ilivyomfanya kutokwa na fahamu papo hapo. Hakutaka aanguke kama mzigo ili kutowashtua wenzake. Alimkamata na kumpeleka chini taratibu, akamlaza chini ya mti.

Akaichukua bunduki iliyokuwa mikononi mwa adui. "Sasa kazi imekuwa rahisi kuliko urahisi wenyewe." Alijisemea.

Tayari alikuwa ameshapunguza mtu mmoja, walibaki watano badala ya sita.

"Tawanyikeni." Amri ilitoka kwa mkubwa wao.

Hilo ndilo alilokuwa akilisubiri. Mmoja wao alipita karibu na alipokuwa Eddy. Akiwa hajui hili wala lile, ghafla Eddy alijitokeza mbele yake. Nia kwanza ilikuwa ni kutia hofu. Mara nyingi hofu humfanya mtu kutokuwa au kuishiwa na nguvu.

**Hilo ndilo alilokuwa akilisubiri. Mmoja wao alipita karibu na alipokuwa Eddy. Akiwa hajui hili wala lile, ghafla Eddy alijitokeza mbele yake. Nia kwanza ilikuwa ni kutia hofu. Mara nyingi hofu humfanya mtu kutokuwa au kuishiwa na nguvu.**

Kabla ya kupiga kelele, lilifuata teke la mdomo ili ashindwe kusema chochote au kupiga kelele kuwasiliana na wenzake. Sekunde chache baadaye teke hilo hilo lilitua kwenye mbavu na kuanguka chini kama mzigo.

Wakati wote huo, Eddy alijua watu hao hawakufa, ila watazinduka baada ya nusu saa au dakika arobaini na tano. Sasa walibaki wanne.

Walikuwa wametwanyika ambavyo Eddy asingeweza kuwapata kiurahisi. Alijibana kwenye mti mmoja mkubwa na kuwa sehemu ya giza lenyewe. Aliimuona mtu mwingine mwenye silaha alinyatia eneo alilokuwa.

Jinsi alibyonyata, Eddy alijua jamaa hajui kama pale kuna mtu. Alikuwa na silaha. Kwa uzoefu wake tu alijua hiyo ndiyo itakuwa silaha ya mwisho kubwa kwa watu wale. Alikuwa na uhakika kama akiipata, basi atakuwa ameshawanyong'onyesha kabisa.

Kama kawaida yake, aliokota kipande cha mti uliokuwa umekauka. Akamrushia, ukampiga usoni.

Jamaa alishtuka na akaanza kufyatua risasi hivyo. Wakati huo Eddy alikuwa ameshalala chini, kabla ya kutambaa kwa kasi hadi alipo jamaa ambaye aliendelea kupiga. Hakumuona Eddy aliyekuwa alitambaa kama nyoka. Akakwanguliwa mtama na kuruka juu, kabla ya kuanguka mtaroni kama gunia.

Bastola ilianguka pembeni. Eddy alijua hawakuwa tena na bastola. Si kawaida kikundi cha wahalifu kama wale wakawa na bunduki zaidi ya mbili. Mara nyingi ni moja au mbili tu. Alitoka haraka alipoifuta na kuichukua. Ilikuwa ni kwa uangalifu zaidi akiwa amekamata bastola aliyoichukua kwa yule ya kwanza, akiwa tayari kuitumia kwa chochote kitakachotokea.

Tayari alikuwa ameshamzimisha mtu wa tatu. Walibaki watatu. Hawakuwa na silaha. Walianza kuona walivyodhani sivyo.

Mmoja alionekana kuanza kukimbia. Ni baada ya kuona wale wenye silaha hawaonekani. Mmoja kapotea ghafla na mwingine ni kama amerushwa kama gunia la mchanga kwenye mtaro na kufikia kiuno.

Eddy alimuona, kabla hajavuka barabara, aliachia risasi moja, iliyompata mguuni. Ya pili ilimpata kwenye mguu mwingine akakaa chini na kushindwa hata kusota.

"Jitokezeni wote mliobaki kwa usalama wenu." Aliunguruma.

Mmoja alijitokeza. Alionekana muoga mno. Alipokaribia alimwambia akae chini. Akakaa. Mwingine alijitokeza. Alipiga hatua kadhaa. Mikono yake ilikuwa juu. Lakini akili yake ilifanya kazi vizuri sana. Nadhani alikuwa hamfahamu vizuri Eddy. Mara nyingi ni hatari zaidi kucheza na adui usiyemjua.

Alidhani alibahatisha tu kuchukua bastola. Alipofika karibu alirusha teke ambalo liliipiga bastola aliyokuwa ameishika Eddy na kuanguka chini.

Eddy alitegemea hilo. Alikuwa na uwezo wa kuikwepesha. Lakini alikuwa anataka kumuona ni mtu wa gani. Kuwanyong'onyesha watu wanne kati ya sita, tayari aliona ni ushindi. Wale wawili waliobaki hawasingeweza kumbabaisha.

Ngumi ilirushwa ambayo ilikusudiwa kutua kwenye taya. Hii aliikwepa. Tayari adui alitambua kuwa mpinzani wake ameangusha bastola, hivyo asingeweza kumfanya lolote. Alikosema. Eddy aliikwepa kwa ustadi iliyomshangaza mtu huyo. Wakati akishangaa, Eddy alirusha mateke mawili yalilokwenda sawia kwenye kwenye kifua cha jamaa yule.

Hapo ndipo alipogundua kuwa hakuwa mbele ya mtu wa kawaida. Ni mjuzi hasa. Akaamua kubadilisha mipigo. Aliachia teke la kuzunguka, ambalo limpata Eddy kwenye mbavu. Alijifanya ameumia sana.

Hakujua kuwa alidanganywa. Eddy ni mpelelezi maarufu nchini Tanzania ambaye amefundishwa vitu vingi vya kikomandoo, hivyo teke lile lisingemtoa kwenye reli.

Aliendа mzima mzima kwa lengo la kutaka kummaliza, baada ya kuona amemlegeza. Alikiona cha moto. Eddy alipeleka mapigo matatu ya karate mbili za kifua na moja ya tumbo, ikamrusha hatua kadhaa nyuma na kuanza kutapika damu.

Tukio lile lilimuogopesha sana mwenzake na kumfanya atetemeke mwili mzima. "Hallo hallo Makao Makuu. Naomba mje na kikosi hapa, kuna kikundi cha wahalifu hapa kilituvamia. Sijajua nia yao, lakini hayo mengine tutayajua ofisini, naomba askari na gari la wagonjwa, pamoja na la kukokota magari mabovu" alipiga simu ofisini kwake.

Saa yake ilimuonyesha imetimua saa tatu usiku. Magari yaliwasili na kuwachukua wote. Yeye hakuondoka.

Alirejea kwenye makaburi alipozikwa Patiyo na Grace. Alimkuta Shani akiwa amelala kifudifudi kama alivyoambiwa. Lakini akiwa anatetemeka kwa hofu.

"Yameisha mpenzi. Tumepona, sasa tunaweza kwenda nyumbani."

"Nimesikia milio ya risasi nikajua wameshakuua mpenzi wangu, niliogopa sana."

"Wasingeweza kumuua mlinzi wa Shani."

"Kwani walitaka kumuua nani?"

"Wote sisi wawili."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# DORTMUND HAIMWACHII HAALAND




**DORTMUND,** Ujerumani

BORUSSIA Dortmund inapanga kubakia na nyota Erling Haaland kwa muda mrefu wakati Mkurugenzi wa Michezo, Michael Zorc akikanusha uvumi kuhusu usajili wake.

Haaland amefurahia wakati mzuri zaidi wa kucheza soka tangu alipoondoka Salzburg na kujiunga Dortmund Januari, mwaka huu huku akihusishwa na Real Madrid, Manchester United na Juventus.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ametwaa tuzo ya Golden Boy mwaka huu kwa kuweka rekodi ya mchezaji aliyefunga mabao 15 kwa haraka zaidi kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati alipofunga bao la uongozi wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Club Brugge, Jumanne iliyopita.

Haaland alimaliza mchezo huo kwa kufunga mabao mawili na kufikisha jumla ya mabao 16 katika mechi 12 za Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kuipiku rekodi ya Ruud van Nistelrooy na Roberto Soldado.

Mchezaji huyo raia wa Norway, ana mabao 10 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu na 17 kwenye mashindano yote kwa msimu wa 2020-21.

Wakati Haaland akiendelea kuwaniwa na timu kubwa za Ulaya, Zorc ameelezea majaliwa ya mchezaji huyo ambaye ana kipengele cha kuuzwa kwa euro milioni 75.

"Nina furaha kwamba Erling Haaland ari yake ipo juu, kwa sababu anacheza vizuri kwa timu yetu na tumeshafanya kazi nzuri," alisema Zorc akiwaambia waandishi wa habari kuelekea mchezo wa leo Jumamosi wa Bundesliga dhidi ya Cologne.

# Mourinho ampa neno Vinicius

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amedai Carlos Vinicius lazima ajifunze kuonyesha thamani yake kwa Tottenham kwenye Ligi Kuu England baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kwenye Ligi ya Europa.

Vinicius alifunga mabao mawili wakati Tottenham ikiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Ludogorets kwenye Ligi ya Europa katika mechi ya Kundi J iliyochezwa juzi Alhamisi na kuwafanya Spurs wakibakia na pointi moja ili kufuzu hatua ya mtoano.

Mabao hayo mawili yalikuwa ya kwanza kwa Vinicius kuifungia Tottenham tangu alipojiunga na klabu hiyo ya jiji la London kwa mkopo wa muda mrefu akitokea kwa miamba wa Ureno, Benfica Oktoba, mwaka jana.

Vinicius amachangia katika mabao matano (mabao mawili na pasi za mwisho tatu) katika mechi nne za Ligi ya Europa kwa Spurs hao msimu huu.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Mourinho alisema amemwambia Vinicius lazima ajifunze kuzoea Ligi Kuu England ili apate mafanikio.

"Hachezi sana, hasa kwenye Ligi Kuu, lakini alitusaidia sisi kushinda mchezo pale kwa West Bromwich Albion na kwenye Ligi ya Europa anafanya vizuri," alisema Mourinho.

"Lilikuwa jambo zuri kwamba alifunga mabao muhimu. Halafu kipindi cha pili akatoa pasi ya mwisho kwa bao la Lucas Moura."







# Arteta: Pepe amemaliza hasira

**MOLDE,** Norway

MIKEL Arteta alifurahishwa kwa kiwango cha Nicolas Pepe wakati Arsenal ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Molde kwenye Ligi ya Europa.

Arteta aliachwa ameghazabishwa na Pepe ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi pale Arsenal, wakati alipoonyeshwa kadi nyekundu kwa kumpiga na mpira kichwani Ezgjan Alioski, walipotoka sare ya bila kufungana na Leeds United, Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alipewa nafasi Alhamisi kwenye Ligi ya Europa na akafunga bao la ufunguzi pale Norway, wakati washikabunduki hao walipofuzu raundi ya 32.

Reiss Nelson alifunga bao la pili na Folarin Balogun akafunga goli lake la kwanza kwa Arsenal na la tatu kwenye mchezo huo kukamilisha ushindi.

"Kwa uhakika nimevutiwa na kiwango chake," alisema Arteta akimzungumzia Pepe. "Kwa kawaida baada ya kuwa na wakati mbaya, unatakiwa kuona vitu chanya kwa haraka sana.

"Niliweza kumwona tangu dakika ya kwanza, kutoka kwenye lugha ya mwili wake, kwamba alikuwa tayari kufanya lolote. Nafikiri alikuwa na kiwango cha kuvutia sana."

# Digne wa Everton kupasuliwa enka

**LONDON,** England

KLABU ya Everton imethibitisha kwamba, Lucas Digne atafanyiwa upasuaji wa kifundo cha mguu baada ya kuumia kwenye mazoezi wiki hii.

Mlinzi huyo wa kushoto, Digne amekuwa na mwanzo mzuri msimu huu, kwa kumlisha mipira James Rodriguez ambaye mara nyingi amekuwa akicheza winga ya kulia na kutengeneza mashambulizi kutokea kushoto.

Katika mechi nane za Ligi Kuu England, msimu huu, Digne ametengeneza nafasi 16, akishika nafasi ya pili nyuma ya James (18) kwa wachezaji wa Everton.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona ametoa pasi za mwisho nne, zikiwamo mbili katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Fulham katika mchezo wake wa mwisho.

Digne ameanza katika kila mchezo wa ligi na amekuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27 aliukosa mchezo wa kichapo wa Newcastle United baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati wakifungwa mabao 2-0 na Southampton Oktoba 25, mwaka huu.

Taarifa ya Everton imesema kwamba, Digne atafanyiwa upasuaji Jumatatu, kabla ya kuanza kujiuguza na haujatwa muda ambao atakuwa nje ya dimba.






# MARADONA AZIKWA NA NDUGU, MARAFIKI TU

Watoto wa nyota wa zamani wa Argentina, Diego Maradona, Dalma ambaye ana umri wa miaka 33 (kushoto) na Giannina (31), wakiwa kwenye majonzi wakati wa mazishi ya baba yao yaliyofanyika kwenye makaburi ya Bella Vista kwenye mji wa Buenos Aires juzi. **PICHA: MTANDAO**

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona amefanyiwa mazishi ya kibinafsi katika mji wa Buenos Aires nchini Argentina siku moja baada ya kufariki dunia.

Jamaa na marafiki wa karibu tu ndio waliohudhuria mazishi yake.

Lakini awali, kundi kubwa la watu lilijitokeza kutoa heshima zao za mwisho, wengi wakiwa wanabubujikwa machozi na kuonyesha upendo kwa gwiji huyo.

Maradona alifariki dunia kwa sababu ya mshtuko wa moyo akiwa na umri wa miaka 60.

Kifo chake kimesababisha watu kuombeleza kote duniani, lakini hakuna walioomboleza kama raia wa nchi yake waliomchukulia kama shujaa wa taifa.

Jeneza la Maradona lilifunikwa bendera ya taifa na fulana ya jezi yenye namba 10, nafasi aliyocheza uwanjani pia jezi hiyo ilikuwa inaonyeshwa kwa umma katika makao ya rais.

Kufikia mchana, foleni ya waliokuwa wamekuja kutoa heshima zao za mwisho ilifika umbali wa zaidi ya kilomita moja na polisi ikakabiliana na waombolezaji walipokuwa wanajaribu kufunga kwa sababu ya muda.

Aidha, kulikuwa na taarifa za waombolezaji kurushiwa mabomu ya kutoa machozi na risasi za mpira.

Maradona alizikwa katika makaburi ya Bella Vista pembeni ya wazazi wake.

# *Pogba ajikatia tamaa kikosini*

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kimataifa wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba, yupo katika wakati mgumu wa maisha yake ya soka.

Pogba anaweka bayana hajapata kuwa katika hali mbaya kama sasa tangu ajiunge na Manchester United.

Mambo yanayomsumbua ni pamoja na kukosa muda wa kutosha wa kucheza chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Amekuwa akiachwa benchi katika mechi kadhaa, ambapo hata akipewa nafasi ya kucheza ufanisi wake umekuwa chini kiasi cha kuwatia simanzi mashabiki wa Mashetani Wekundu hao.

Pamoja na kuwa chini kwa kiwango, Kocha wa Timu ya Taifa ya Ufaransa – Les Bleus, Didier Deschamps alimwita kikosini na kumpa muda wa kucheza.

Hivyo, walau anasema Pogba ni pumzi mpya inayompa msukumo wa kuanza tena kukipiga kwa nguvu akiwa na United.

Nafasi yake kwa sasa pale United imechukuliwa na Scott McTominay na Fred wanaocheza na Bruno Fernandes.

"Sikupata kujua wala kuwa na uzoefu wa kipindi kigumu kama hiki tangu nianze soka ya kulipwa. Timu ya Taifa ya Ufaransa ni liwazo kwangu na pumzi mpya nzuri. Kundi hili si la kawaida, ni la aina yake hasa," alisema Pogba mwenye umri wa miaka 27 akiambia RTL.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATAKIWA KUBAKIA LALIGA

●●● Rais wa ligi hiyo afunguka pia mpango wa kuwarejesha Mourinho, Guardiola, Ronaldo...

**MADRID,** Hispania

RAIS wa LaLiga, Javier Tebas, amesema anataka nyota wa Barcelona, Lionel Messi kubakia Hispania, kama ambavyo anataka Cristiano Ronaldo, Jose Mourinho, Pep Guardiola na Jurgen Klopp kuwapo kwenye ligi hiyo.

**Majaliwa ya Messi bado yamebakia mjadala muhimu kwa miamba wa LaLiga Barcelona, baada ya nyota huyo kuomba kuondoka baada ya kuwa na msimu mbaya wa 2019-20.**

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alikuwa anatajwa kujiunga na matajiri wa Ligi Kuu England, Manchester City kabla ya kuamua kubakia nchini Hispania, ingawa amekuwa akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain na InterMilan.

Tebas aliulizwa kuhusu majaliwa ya Messi na alipuuzia athari ya uwezekano wa nahodha huyo wa Argentina kuondoka. "Namtaka Messi kwenye LaLiga, kama ambavyo nataka (Kocha Mkuu wa Tottenham) Mourinho, (Kocha wa City) Guardiola, (Kocha wa Liverpool) Klopp, (Nyota wa Juventus) Cristiano...," Tebas alisema kwenye kongamano la soka la Dunia.

"Watatusaidia kukua.

"Sio muhimu sana. Wao sio muhimu sana kama watu wanavyosema. Neymar aliondoka. Ni muhimu kuwa na mikakati, mchezaji anaweza kukusaidia, lakini sio muhimu.

"Tuna dili kubwa kwa misimu minne ijayo. Inaweza kuathiri udhamini kwa kiasi fulani, lakini tumefaya kazi kubwa katika kuitangaza ligi yetu na umuhimu wake.

"Natumaini kwamba, Messi, ambaye ni mchezaji bora zaidi, atamalizia soka lake hapa."

Messi ametumia kipindi chake karibia chote cha kucheza soka pale Camp Nou, tangu alipotokea timu ya vijana ya Barca mwaka 2004.

Tangu kuanza kucheza hapo, Messi amekuwa mfungaji wa wakati wote na ameshinda mataji 34 yakiwamo 10 ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu wa 2020-21, Messi amefunga mabao matatu kwenye mehi nane za LaLiga na Barca ipo nafasi ya 13 kwenye msimamo, wakiwa amepitwa pointi 12 na Real Sociedad.

Messi amefunga mabao sita katika mashindano yote aliyocheza chini ya kocha Ronald Koeman msimu huu.

## ZISIKUPITE

### MANE ATAJWA BARCELONA

BARCELONA huenda ikamnyatia mshambuliaji wa Liverpool raia wa Senegal, Sadio Mane,28, au kiungo wa kati wa Uholanzi, Gini Wijnaldum mwenye miaka 30, baada ya kipengele katika makubaliano yaliyowezesha Philippe Coutinho kwenda Nou Camp kumalizika. ***(Star)***

### NEYMAR KUREJESHWA

MGOMBEA urais wa Barcelona, Emili Rousaud amesema kama atachaguliwa atasajili "wachezaji wawili wazuri, mmoja wao akiwa Neymar" 28, ambaye aliweka rekodi ya dunia ya uhamisho kutoka Barca hadi Paris St Germain mwaka 2017. ***(Marca)***

### LYON YAMTEMA AOUAR

LYON imemtema kikosini, Houssem Aouar anayewaniwa na Arsenal kwenye mchezo wa leo Jumamosi dhidi ya Reims baada ya kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, kukataa kufanya mazoezi baada ya kuwekwa benchi na kutotumika kwenye mchezo dhidi ya Angers. ***(L'Equipe via Mirror)***

### UNITED YAMWOTA DEMBELE

MANCHESTER United haijakata tamaa ya kumsajili nyota wa Barcelona, Ousmane Dembele, lakini watajaribu kukubali kwanza kumchukua kwa mkopo raia huyo wa Ufaransa mwenye miaka 23. ***(Sport)***

### JUVE YAMWINDA DE BEEK

JUVENTUS inafuatilia kwa karibu hali ya nyota wa kimataifa wa Uholanzi, Donny van de Beek pale Manchester United, baada ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23 kushindwa kupata nafasi ya kuanza mara kwa mara tangu atue hapo kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomercato)***

### GIMENEZ ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inaangalia uwezekano wa kumsajili mlinzi wa kati wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Uruguay, Jose Gimenez, mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

### SPURS YAMFUATA GRAY

KLABU ya Tottenham Hotspur inajipanga kumsajilili winga wa Leicester, Demarai Gray, 24, kwa uhamisho huru Januari. ***(Express)***

### SHAQIRI, ORIGI SOKONI

LIVERPOOL inaweza kupata pauni milioni 30 kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari kwa kumuuza kiungo wa kimataifa wa Uswisi, Xherdan Shaqiri, 29, na straika wa Ubelgiji, Divock Origi, 25. ***(Express)***

### DONNARUMMA KIMEELEWEKA

GOLIKIPA wa Italia, Gianluigi Donnarumma, 21, anakaribia kusaini mkataba na AC Milan. ***(Calciomercato)***

### FOSU-MENSAH SAFI

MANCHESTER United imetoa ofa ya mkataba mpya kwa mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi Timothy Fosu-Mensah, 22, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

## Masau aendelea ‘kuibeza’ Simba

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, ameonyesha kufurahishwa na ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya Tanzania Prisons na kutamba kikosi chake kimewafunga ‘wababe’ wa Simba.

Masau alisema matokeo hayo yanadhihirisha wao ni wazuri zaidi kwa sababu baada ya kuifunga Simba, pia imeifunga Tanzania Prisons ambayo iliwachapa pia mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara.

“Nikiitaja Simba watu wananishangaa, lakini lazima nifananishe vitu vingi na Simba kwa sababu wao ndiyo mabingwa watetezi wa Ligi Kuu. Wao ndiyo wanaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, lakini wao ndiyo wanaosadikiwa kuwa na kikosi kizuri zaidi hapa nchini, ndiyo maana unaona nafananisha vitu vingi na timu hiyo.” Alisema Masau.

Alisema Simba ndiyo timu inayoogopeka kwa sasa kwenye Ligi Kuu, lakini wao Ruvu Shooting walipata ushindi dhidi ya vigogo hao, hivyo wanaendelea kujivunia.

Ruvu Shooting kesho itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani kuwakaribisha Kagera Sugar na endapo itashinda mchezo huo, itafikisha  pointi 25 na kuiacha Simba ikiwa na pointi 23.

Simba haitocheza mechi yoyote ya ligi wiki hii kutokana na kuiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo inaanzia ugenini Nigeria dhidi ya Plateau United.

## Mlandege, Sfaxien majaribuni Afrika

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege FC wanatarajia kuwakaribisha Waarabu wa Tunisia CS Sfaxien katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan.

Akizungumzia na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mlandege, Abdulmutik Haji alisema wamejiandaa vyema kusaka ushindi katika mechi hiyo ili wajitengenezee nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Haji alisema wamejipanga kucheza kwa tahadhari ili wasipoteze mchezo huo wa hapa nyumbani ili wawe kwenye mazingira ya kwenda kumalizika vizuri watakapokwenda katika mchezo wa marudiano.

Nahodha wa Mlandege, Sabri Ramadhani ‘China’ alisema wamejiandaa kuanza vyema kampeni hiyo ya kimataifa na kisaikolojia wachezaji wote wamejipanga kupata matokeo chanya ndani ya dakika 90 za kwanza.

Naye Kocha Mkuu wa CS Sfaxien, Anis Boujelbene alisema malengo yake kupata ushindi katika mechi hiyo ya kwanza na anaifahamu Mlandege ni timu kubwa hapa Zanzibar.

“Timu yetu ni bingwa wa Tunisia na Mlandege ni mabingwa wa Zanzibar, naamini hii ni timu nzuri na timu kali kulingana na tulivyoifuatilia kupitia video zao mbalimbali ambazo tumebahatika kuziona,” alisema kocha huyo.

# NAMUNGO YATAMBA KUANZA VYEMA CAF

**Na Saada Akida**

USHINDI ndio neno lililoko kwenye mdomo wa Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, kuelekea katika mechi ya kimataifa ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Rabita kutoka Sudan Kusini itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini, Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema anahitaji kumaliza mechi hiyo mapema kwa kupata ushindi ambao utawaweka kwenye nafasi nzuri.**

Morocco alisema atahakikisha anaingia na mbinu mpya ili kuwamaliza wapinzani wao  Al Rabita FC hapa nyumbani kwa sababu ya ‘kujisafishia njia’ ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

“Natakiwa kumaliza mechi mapema, nipate ushindi mkubwa, kizuri zaidi tunaanzia nyumbani, saikolojia ya wachezaji wangu ipo vizuri, bado ninaendelea kufanyia kazi upungufu mdogo mdogo ya safu ya ushambuliaji,” alisema Morocco.

Aliongeza amebaini kuwapo na mabadiliko katika safu ya ushambuliaji na ana imani watafikia malengo kwa sababu anahitaji kuvuka katika hatua hiyo ya kwanza ya michuano hiyo.

Naye Katibu wa Namungo, Ally Suleiman, alisema wenyeji wao tayari wameshawasili nchini tangu Jumatano na leo wanatarajiwa kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Azam Complex ambao utatumika katika michuano hiyo.

“Wenyeji wao wamewasili ni kikosi cha watu 26, suala la mashabiki kuingia uwanjani tunasubiri taarifa kutoka katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambao ndio watatupa mwongozo wa CAF,” alisema Ally.

Namungo itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na mchezo wa leo utakuwa ni wa pili kwa Morocco ambaye alirithi mikoba ya Hitimana Thiery.

Klabu hiyo ya Lindi ilipata tiketi ya kushiriki mashindano hayo ya kimataifa ikiwa ni mara yake ya kwanza baada ya kucheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba, ambayo ilishinda kombe hilo pamoja na taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi jijini Abuja, Nigeria ili kujiandaa na mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United itakayochezwa kesho kwenye Mji wa Jos nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# *Kocha Julio ajipanga kufuzu Afcon*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20), Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, (Ngorongoro Heroes), Jamhuri Kihwelo ‘Julio’ amesema malengo yake makubwa ni kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Afrika (Afcon).

Ngorongoro Heroes imetinga hatua hiyo baada ya kuifunga Somalia mabao 8-1 na hivyo kuongoza katika Kundi A kwenye michuano hiyo inayoendelea jijini, Arusha kwa kushirikisha nchi tisa.

Akizungumza na gazeti hili, Julio, alisema wamejiandaa kupambana katika mechi inayofuata ili kuhakikisha wanapata tiketi ya kushiriki fainali hizo za Afcon.

Julio alisema mechi zote za mashindano hayo ni ngumu na zina ushindani huku akiwataka wadau waachane na mawazo kwamba walipangwa kundi jepesi.

“Tumetumia nguvu kubwa kufika hatua hii, hakuna mechi nyepesi, tuachane na mawazo ya kufikiria Somalia, au Djibouti ni timu nyepesi, wamebadilika, sio kama ilivyokuwa zamani, sisi tutaendelea kujipanga ili kutimiza malengo yetu ya kwenda Afcon,” alisema Julio.

Mashindano hayo yanatarajiwa kuendelea tena keshokutwa Jumatatu kwa mechi mbili za hatua ya nusu fainali wakati fainali ya michuano hiyo itafanyika Desemba 2, mwaka huu.

Ngorongoro Heroes ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambayo mwaka jana ilifanyika kwenye Uwanja wa Njeri, ulioko katika Mji wa Jinja nchini Uganda.

# Michezo

Jumamosi Novemba 28, 2020

Nipashe




Messi atakiwa kubakia LaLiga UKURASA 22



Rais wa Argentina, Alberto Fernandez (kushoto), akiwa na rafiki yake wa kike, Fabiola Yanez, wakitoa heshima ya mwisho katika jeneza la nyota wa zamani wa nchi hiyo, Diego Maradona, ambaye alizikwa kwenye makaburi ya Bella Vista mjini Buenos Aires juzi. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATAMBA KUENDELEZA DOZI

## Ni kuelekea mechi yao dhidi ya JKT Tanzania, Maafande wafunguka 'siku hazifanani'...

**Na Somoe Ng'itu**

HAKUNA kulala! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi, Cedriz Kaze, kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya 'Maafande' wa JKT Tanzania unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara zina ushindani lakini amekiandaa kikosi chake kupata pointi tatu ili wafikie malengo ya kutwaa taji la ligi hiyo kwa msimu huu wa 2020/21.**

Kaze alisema wachezaji wake wameendelea kuimarika tofauti na alivyowakuta ingawa kuna baadhi ya nyota wake bado hawajafikia viwango anavyovihitaji katika kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi kwenye ligi hiyo.

Kocha huyo alisema amekuwa akiwakumbusha washambuliaji wake kuongeza umakini kila wanapokuwa na mpira na vile vile kutulia wanapokaribia lango la wapinzani wao, kwa sababu wakifanya hivyo watajiweka kwenye mazingira mazuri ya kuondoka na ushindi.

"Wachezaji wamefanya mazoezi vizuri, wanajua malengo yetu ya pamoja, timu inahitaji ushindi, ili upate ushindi na pointi tatu ni lazima tuendelee kupambana, tucheze kwa kasi, hatutakiwi kujisahau, hii ligi hakuna kulala," alisema Kaze.

Aliongeza benchi lake la ufundi bado linaendelea kuwapa mbinu mbadala washambuliaji wao kwa sababu wanahitaji kuona wanapata idadi nzuri ya mabao na pia kupata ushindi wa mapema ili kujiondoa kwenye hofu ya kuharibu mchezo.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema kikosi cha timu yao kiko kamili na tayari kuendelea na mbio za kuwania ubingwa wa ligi msimu huu.

Bumbuli alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na kamwe hawataidharau timu yoyote watakayokutana nao kwa sababu wanataka kukamilisha malengo yao.

"Sisi tunafukuzia ubingwa, wengine wafukuze makocha, kesho (leo), tena Wananchi tuna jambo letu," alisema Bumbuli.

Kocha wa JKT Tanzania, Abdallah Mohammed 'Bares' aliliambia gazeti hili Yanga wanatakiwa kujipanga na wasitegemee mteremko katika mechi hiyo kwa sababu siku hazifanani.

"Tumeshafika mjini, tumekuja hapa kwa kazi moja ya kutafuta ushindi, ingawa tunajua pia wapinzani wetu wanautaka ushindi huo, tutarajie kuona mechi ngumu na yenye ushindani kwa kila upande, " alisema kocha huyo.

Kocha huyo aliongeza amewaambia wachezaji wake wacheze kwa tahadhari na umakini kutokana na wapinzani wao kutoonyesha kukata tamaa hadi dakika ya mwisho ya mchezo.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Mbeya City dhidi ya Mtibwa Sugar wakati Dodoma Jiji FC itawakaribisha Ihefu FC kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma wakati kesho Ruvu Shooting itavaana na Mwadui FC huku Coastal Union itawafuata Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

***Wakati huo huo***, kikosi cha Azam FC kinatarajia kuanza safari ya kuelekea Musoma leo kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Biashara United utakaochezwa keshokutwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Karume mkoani Mara.

# Simba kumaliza kibarua ugenini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba kinaondoka Abuja leo kuelekea katika Mji wa Jos, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Matola amesema kikosi chao kiko imara na kinataka kumaliza kazi ugenini.

Simba inatarajia kukutana na wenyeji, Plateau United katika mechi ya kwanza ya hatua ya awali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Jos kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jana, Matola alisema wachezaji wote wa Simba wako katika hali nzuri na kila mmoja ameahidi kucheza vyema ili kuipa timu hiyo matokeo chanya kwenye mchezo huo wa kwanza kwa ajili ya kuifanya mechi ya marudiano kuwa nyepesi.

Matola alisema hali ya hewa ya Abuja haijawasumbua wachezaji wao na wamefanya mazoezi kwa kufuata programu zote zilizoandaliwa na benchi la ufundi ambalo liko chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

"Tuko vizuri kila idara, tunatarajia kuondoka hapa (Abuja), saa 9:00 mchana (sawa na saa 11:00 jioni Tanzania), kuelekea katika mji wa Jos, tumeambiwa huko kuna baridi kama Arusha, halitatupa shida, tunaenda huko kupambana, vijana wameahidi kumaliza kazi huku, kikubwa tuombeeni dua tutekeleze tulichokipanga," alisema Matola.

Aliongeza tayari wameshaanza 'kuwasoma' wapinzani wao kwa kuanza baadhi ya mechi walizocheza ili kufahamu ubora na udhaifu wao na wataendelea kufanya hivyo leo kwa ajili ya kujiimarisha kabla ya kuteremka uwanjani.

"Hawa hawajacheza mechi muda mrefu, lakini kuna mechi yao walicheza na Enyimba tumeifuatilia, imetusaidia kuwafahamu, tunaamini tutakuwa na mchezo mzuri na wenye matokeo bora kwetu," Matola, nahodha na kiungo wa zamani wa Simba alisema.

Baada ya mechi hiyo, Simba itarejea nyumbani tayari kuwasubiri Wanigeria hao katika mchezo wa marudiano utakaochezwa kati ya Desemba 4 na 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >